# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

## FEBUARI 2024

# YALIYOMO


*SEHEMU YA KWANZA* 1

UTANGULIZI 1

Muundo wa Kamati ya Bajeti 2

*SEHEMU YA PILI* *4*

TATHMINI YA MWENENDO WA UKUAJI WA HALI YA UCHUMI 4

Mfumko wa Bei 4

Mwenendo wa Sarafu ya Tanzania 4

Idadi ya Watalii 5

Maoni na Ushauri wa Kamati 6

*SEHEMU YA TATU* *8*

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/2022 NA NUSU MWAKA WA FEDHA 2022/2023 (JULAI – DISEMBA 2022/2023) 8

Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2022/2023 8

Utekelezaji wa Bajeti kwa Nusu Mwaka wa Fedha 2023/2024 8

Deni la Taifa 9

Maoni na Ushauri wa Kamati 10

*SEHEMU YA NNE* *12*

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 .12

Mapato ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango 12

Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango 13

Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti za Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa kipindi cha Julai - Septemba 2023/2024KIKODI PEMBA 14

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) 14

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar 16

Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) 18

Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) 21

Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) 22

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) 24

*SEHEMU YA TANO* *12*

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA 27

SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC) 27

KAMPUNI YA UUNGANISHAJI NA USAMBAZAJI WA MAUDHUI ZANZIBAR (ZMUX) 28

MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA) 30

WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR 32

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI (OCGS) 34

KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR (ZAFICO) 36

SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR (ZHC) 37

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC) 38

WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR (ZBA) 40

WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR (ZEEA) 41

SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO) 42

SHIRIKA LA BANDARI (ZPC) 44
MTHAMINI MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR 45

*SEHEMU YA SITA* *47*

**TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA PROGRAMU MBALI MBALI** **47**
MRADI WA ELIMU YA JUU KWA MABADILIKO YA KIUCHUMI (HEET) ZANZIBAR 47
MRADI WA UJENZI WA MASOKO YA MWANAKWEREKWE, JUMBI NA CHUINI 49
MRADI WA UIMARISHAJI WA MIUNDOMBINU YA SKULI 51
MRADI WA UJENZI WA MAHKAMA ZA MIKOA 52
MRADI WA UKARABATI WA MAGHALA NA UHIFADHI WA CHAKULA 52
MRADI WA UANZISHWAJI WA KITUO CHA KUHIFADHIA DATA ZA MAFUTA NA GESI ASILIA 54
MRADI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI MAJI ZANZIBAR 55
MRADI WA UHUISHAJI NA UIMARISHAJI WA MFUMO WA USAMBAZAJI MAJI ZANZIBAR 57
PROGRAMU YA KUIMARISHA VIWANJA VYA NDEGE 58
MRADI WA UJENZI WA NYUMBA ZA WAFANYAKAZI KATIKA HOSPITALI ZA WILAYA NA MKOA 59
PROGRAMU YA UJENZI WA BARABARA KUU PAMOJA NA UJENZI WA BARABARA ZA NDANI 60
PROGRAMU YA UJENZI WA OFISI ZA SERIKALI 62
MPANGO WA UNUNUZI WA VYOMBO VYA USAFIRI (GARI) 63
MRADI WA MJI SALAMA 65
MRADI WA UJENZI WA OFISI ZA MASHEHA ZANZIBAR 65
MRADI WA UJENZI WA NYUMBA NA MAHANGA YA CHUO CHA MAFUNZO 66
PROGRAMU YA KUIMARISHA VIWANJA VYA MICHEZO 67
MRADI WA BANDARI JUMUISHI MANGAPWANI 69

*SEHEMU YA SABA* *71*

**TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA** **71**
Tathmini ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bajeti kwa Mabaraza ya Miji na Manispaa kwa Upande wa Pemba 71

*SEHEMU YA NANE* *74*

**HITIMISHO** **74**

# SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Kamati ya Bajeti ni moja ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zilizoundwa rasmi chini ya Kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Baraza, Toleo la Mwaka 2020. Kamati hii inatekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizo. Zaidi ya hayo, Kamati huzingatia Katiba, Sheria na miongozo mbali mbali ya nchi katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Majukumu ya Kamati ya Bajeti yaliyoainishwa katika Kanuni hizo ni kama yafuatayo:

i. Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu uandaaji wa mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kila mwaka;
ii. Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;
iii. Kufanya utafiti na uchambuzi kuhusu sera za kodi, sera za fedha na sera za kiuhasibu zilizopendekezwa na Serikali;
iv. Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali na mapendekezo ya hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti;
v. Kutoa ushauri wa jumla kuhusu bajeti ya Serikali kwa Baraza na Kamati za Kudumu za Baraza;
vi. Kuchambua na kutoa maoni na ushauri kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaopendekezwa na Serikali;
vii. Kuchambua hoja zitakazojitokeza kwenye Kamati za Kudumu za Baraza wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa ajili ya kuishauri Serikali;
viii. Kuchambua mapendekezo ya jumla ya Serikali kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi;
ix. Kufikiria na kuchunguza Mswada wa Makadirio na Mapato ya matumizi ya mwaka;
x. Kuchambua mapendekezo ya Serikali endapo itataka kuwasilisha katika Baraza Mswada wa Matumizi ya Nyongeza kwa mujibu wa kanuni ya 102 ya

Kanuni hizi; na

xi. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia na kutathmini taarifa ya Wizara juu ya utekelezaji wa maagizo hayo na kuwasilisha Barazani maoni ya Kamati kuhusu taarifa hiyo.

Ili kutekeleza majukumu yake, Kamati ilikutana na Wizara, Taasisi, Mamlaka, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Idara Maalum za SMZ pamoja na wadau mbali mbali kwa lengo la kupokea taarifa za utendaji kazi na kupokea maoni mbali mbali.

## Muundo wa Kamati ya Bajeti

Kamati ya Bajeti inajumuisha Wajumbe nane (8) na Makatibu Kamati wanne (4) kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdalla Mussa Mjumbe
4. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha Mjumbe
5. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad Mjumbe
6. Mhe. Rukia Omar Ramadhan Mjumbe
7. Mhe. Suleiman Masoud Makame Mjumbe
8. Mhe. Yussuf Hassan Iddi Mjumbe
9. Ndg. Asha Said Mohamed Katibu
10. Ndg. Abass Vuai Mohammed Katibu
11. Ndg. Husna Rajab Othman Katibu
12. Ndg. Shaib Fadhil Shaib Katibu

Ripoti hii ya Kamati ya Bajeti ina Sehemu Kuu Nane (8). **Sehemu ya Kwanza** ni Utangulizi; **Sehemu ya Pili** ni Tathmini ya Mwenendo wa Ukuaji wa Hali ya Uchumi Zanzibar; **Sehemu ya Tatu** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023 na kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka wa Fedha

2023/2024; **Sehemu ya Nne** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa Kipindi cha Julai – Disemba Mwaka 2023/2024; **Sehemu ya Tano** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Taasisi na Mashirika ya Umma; **Sehemu ya Sita** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; **Sehemu ya Saba** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; na **Sehemu ya Nane** ni Hitimisho.

# SEHEMU YA PILI

## TATHMINI YA MWENENDO WA UKUAJI WA HALI YA UCHUMI

### Mfumko wa Bei

Mfumko wa bei Zanzibar umekuwa wa wastani katika miaka ya hivi karibuni.

Katika mwaka 2023 mfumko wa bei Zanzibar umefikia asilimia 6.9. Mwaka 2022, mfumko wa bei ulikuwa asilimia 5.1, ikilinganishwa na mfumko wa bei wa asilimia 1.7 mwaka 2021. Ni matarajio ya Kamati ya Bajeti kwamba mfumko wa bei utaendelea kudhibitiwa ili uendelee kuwa wa wastani na wa tarakimu moja katika miaka ya ijayo.

**Jadweli Nam. 1: Mfumko wa Bei kwa kila mwezi kwa mwaka 2022 na 2023**

| **Mwezi** | **Mfumko wa Bei (Asilimia)** | |
|---|---|---|
| | **2022** | **2023** |
| Januari | 2.8 | 8.4 |
| Februari | 2.9 | 7.8 |
| Machi | 3.5 | 7.1 |
| Aprili | 4.1 | 7.5 |
| Mei | 3.7 | 6.4 |
| Juni | 4.2 | 6.5 |
| Julai | 4.5 | 6.7 |
| Agosti | 5.4 | 6.8 |
| Septemba | 7.0 | 7.5 |
| Oktoba | 7.3 | 6.5 |
| Novemba | 7.8 | 6.3 |
| Disemba | 8.1 | 5.5 |
| **Wastani kwa Mwaka** | **5.1** | **6.9** |

**Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (2024)**

**Mwenendo wa Sarafu ya Tanzania**

Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 2,506.03 katika kipindi cha Disemba mwaka 2023, ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,308.89 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, Shilingi ya Tanzania ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 15.96 kwa Shilingi moja ya Kenya katika kipindi cha Disemba mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa TZS 18.71 kwa Shilingi moja ya Kenya katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kadhalika, katika kipindi hicho cha Disemba 2023, Shilingi ya Tanzania ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 0.65 kwa shilingi moja ya Uganda

ikilinganishwa na wastani wa TZS 0.61 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

Sarafu ya Tanzania imepungua thamani yake dhidi ya sarafu nyingine za kigeni katika miezi ya hivi karibuni. Hii inasababisha ongezeko la gharama za uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kutokana na upungufu wa Dola ya Marekani. Kamati inaipongeza Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha upatikanaji wa fedha hizo za kigeni ili kuwasaidia wafanyabiashara kuweza kuagiza bidhaa muhimu nje ya nchi hususan ambazo hazizalishwi katika nchi yetu. **(Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania)**

## Idadi ya Watalii

Idadi ya watalii wanaotembelea Zanzibar imeongezeka kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni. Mwaka 2023, idadi ya watalii ilikuwa 638,498, ikilinganishwa na 544,233 mwaka 2022. Kuongezeka kwa idadi ya watalii kwa kiasi kikubwa kunachangiwa na juhudi za Serikali katika kuitangaza Zanzibar sambamba na kujenga miundombinu bpra na kuimarisha huduma kwa watalii.

**Jadweli Nam. 2: Idadi ya Watalii kwa kila mwezi kwa mwaka 2022 na 2023**

| **Mwezi** | **Idadi ya Watalii** | |
|---|---|---|
| | **2022** | **2023** |
| Januari | 42,443 | 68,813 |
| Februari | 46,995 | 65,430 |
| Machi | 38,762 | 45,915 |
| Aprili | 20,540 | 27,666 |
| Mei | 20,450 | 26,620 |
| Juni | 34,013 | 47,595 |
| Julai | 58,157 | 58,711 |
| Agosti | 61,388 | 61,466 |
| Septemba | 46,338 | 53,839 |

| | | |
|---|---|---|
| Oktoba | 57,547 | 54,961 |
| Novemba | 55,150 | 57,296 |
| Disemba | 66,720 | 70,186 |
| **Jumla** | **548,503** | **638,498** |

**Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (2024)**

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua zifuatazo ili kuendelea kuimarisha hali ya uchumi wa Zanzibar:

i. Kuweka mikakati mahsusi ya kuimarisha uzalishaji wa ndani ili kupunguza utegemezi wa uagizaji hususan kwa zile bidhaa ambazo tunaweza kuzalisha katika nchi yetu.
ii. Kuendelea kuimarisha miundombinu ya msingi, kama vile barabara, viwanja vya ndege, na bandari.
iii. Kuendelea na juhudi za kuvutia uwekezaji wa kigeni ili kuleta mitaji nchini.
iv. Kuendelea kuimarisha huduma ya jamii hususan elimu na afya.
v. Kuendelea na juhudi madhubuti za kuzalisha ajira kama vile kuimarisha mfumo wa mafunzo ya amali ili kuzalisha nguvu kazi yenye ujuzi ambao unahitajika katika sekta za uzalishaji, kukuza maendeleo ya viwanda vya ndani ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma, na kuimarisha mazingira ya biashara ili kufanya iwe rahisi kwa kampuni kuanzisha na kufanya biashara Zanzibar.

## SEHEMU YA TATU

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/2023 NA KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 2,572.7 bilioni na mapato halisi yalikuwa TZS 1,590.3 bilioni sawa na asilimia 61.8 ya makadirio ya mapato. Serikali imefanikiwa kuongeza ukusanyaji wa mapato halisi kwa asilimia 10.8 ikilinganishwa TZS 1,434.9 bilioni zilizokusanywa mwaka wa fedha uliopita wa 2021/2022. Ukuaji huu wa mapato uliwezeshwa na ukuaji wa uchumi, pamoja na hatua mbali mbali za Serikali za kuongeza mapato ya ndani.

Kwa upande wa matumizi, Serikali ilipanga kutumia jumla ya TZS 2,572.7 bilioni, ikiwa ni pamoja na TZS 1,220.5 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na TZS 1,352.2 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Hata hivyo, matumizi halisi yalikuwa TZS 1,453.7 bilioni. Kati ya kiasi hicho, TZS 993.0 bilioni zilitumika

kwa matumizi ya kawaida, na TZS 460.7 bilioni zilitumika kwa matumizi ya maendeleo.

Serikali iliendelea kuimarisha miundombinu ya msingi, elimu na afya. Katika kipindi hiki, Serikali ilienda na ujenzi wa miradi mbali mbali ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara kuu na za ndani, ujenzi wa viwanja vya ndege, ujenzi wa miundombinu ya maji na nishati.

### Utekelezaji wa Bajeti kwa Nusu Mwaka wa Fedha 2023/2024 (Julai – Disemba 2023/2024)

Katika nusu mwaka wa fedha 2023/2024 (Julai – Disemba 2023/2024), Serikali ilifanikiwa kukusanya jumla ya TZS 1,660.67 bilioni sawa na asilimia 58 ya makadirio ya TZS 2,840.85 bilioni kwa mwaka. Aidha, mapato haya ni sawa asilimia 141 ya mapato halisi ya TZS 683.36 bilioni kwa kipindi hichi katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Matumizi halisi ya Serikali katika kipindi hiki ni TZS 1,431.94 bilioni, ambapo TZS 588.78 bilioni zimetumika kwa matumizi ya kawaida na TZS 843.16 bilioni zimetumika kwa matumizi ya maendeleo.

Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa nusu mwaka wa fedha 2023/2024, kumekuwepo na baadhi ya changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na ukuaji wa mfumko wa bei, ambao uliongezeka kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2022 hadi kufikia wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2023. Ukuaji huu wa mfumuko wa bei ulisababishwa na kupungua kwa thamani ya fedha za umma, na hivyo kusababisha ongezeko la gharama za miradi ya maendeleo. Changamoto nyengine ni kupungua kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani ambayo inatumika sana kununua bidhaa nje ya nchi. Changamoto hii imesababishwa na upungufu wa upatikanaji wa Dola ya Marekani katika masoko ya kubadilisha fedha.

## Deni la Taifa

Deni la Taifa la Zanzibar limekuwa likiongezeka kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni. Hadi kufikia Disemba 2023, Deni la Taifa lilikuwa TZS 820.0 bilioni. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 147 ukilinganisha na deni la TZS 331.9 bilioni lililoripotiwa Disemba mwaka 2022. Aidha, kwa upande wa Deni la Nje linalodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi kufikia Disemba, 2023 lilikuwa TZS 2,562.8 bilioni. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 8.2 ukilinganisha na deni la TZS 2,368.1 bilioni lililoripotiwa Disemba mwaka 2022.

Kamati imeelezwa kwamba, ukuaji huu wa Deni la Taifa la Zanzibar umetokana na sababu mbali mbali, ikiwa ni pamoja na uwekezaji katika miradi ya maendeleo. Serikali imewekeza sana katika miradi ya maendeleo katika miaka ya hivi karibuni, na hii imesababisha kuongezeka kwa gharama za Serikali. Sababu nyengine ni kiwango cha mapato ya ndani bado hakitoshelezi kugharamia miradi ya maendeleo. Hii inasababisha Serikali kutegemea misaada na mikopo ya nje ili kugharamia miradi ya maendeleo.

Mikopo hii ikitumika kwa ufanisi na weledi inaweza kusaidia kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo inaweza kusaidia kukuza uchumi wa nchi yetu. Aidha, inaweza kusaidia kuongeza upatikanaji wa ajira Zanzibar.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua mbali mbali ili kuimarisha utekelezaji wa Bajeti za Serikali kama ifuatavyo:

i. Ili kuwa na utekelezaji mzuri wa bajeti, Serikali inapaswa kuimarisha sekta binafsi na kuipa nguvu ili kuongeza uzalishaji wa ndani ambao mwisho wa siku ni chanzo cha mapato ya Serikali. Hatua hii itasaidia kupunguza nakisi ya bajeti kwa kuimarisha mapato ya ndani.
ii. Serikali iendelee na juhudi za kuimarisha nidhamu ya matumizi kwa taasisi

za umma ili kudhibiti uvujaji wa mapato.

iii. Serikali iendelee kuimarisha vyanzo vya mapato ya ndani na kupunguza utegemezi kutoka nje na kuanza kutekeleza hatua za kujitegemea kibajeti taratibu.

iv. Kuongeza mapato ya Serikali kwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi. Kwa kiasi kikubwa, ukusanyaji wa mapato ya kodi umeimarika jambo ambalo Kamati inaipongeza sana Serikali. Lakini ipo haja sasa, Serikali kuweka mikakati katika kuimarisha mapato yasiyokuwa ya kodi.

v. Kuongeza uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma kwa kuendelea kuimarisha hatua za ufuatiliaji na tathmini ya matumizi ya fedha za umma.

## SEHEMU YA NNE

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### Mapato ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango

Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imejumuisha mafungu makuu sita (6) ambayo ni OR- Fedha na Mipango F01, Mfuko Mkuu wa Serikali F02, Tume ya Mipango F03, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali F04, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali F05 na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali F06. Mafungu hayo yanaundwa na Idara ishirini na tatu (23), Taasisi saba (7) na Ofisi tano (5) za Pemba.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ilikadiriwa kukusanya TZS 2,768 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 11 ya makadirio ya kukusanya TZS 2,498 bilioni ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imekusanya TZS 1,611 bilioni sawa na asilimia 95 ya makadirio ya kukusanya TZS 1,688 bilioni. Mapato haya ya TZS 1,611 bilioni yanajumuisha mapato ya Fungu F01 TZS 1051 bilioni, Fungu F04 TZS 40.577 milioni na Fungu F05 TZS 501.89 bilioni.

Mapato ya Fungu F01 yamejumuisha mapato ya kodi yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa upande wa Zanzibar. Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, mapato yaliyokusanywa na ZRA yamefikia TZS 351.768 bilioni sawa na asilimia 105 ya makadirio ya kukusanya TZS 335.382 bilioni. Kwa upande wa TRA imekusanya TZS 252.932 bilioni sawa na asilimia 101 ya makadirio ya TZS 250.754 bilioni. Aidha, mapato yasiyokuwa ya kodi kupitia Fungu (F01) imekusanya TZS 447.227

bilioni sawa na asilimia 119 ya makadirio ya TZS 375.633 bilioni katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024.

Fungu F04 limekusanya TZS 40.57 milioni sawa na asilimia 69 ya makadirio ya kukusanya TZS 58.70 milioni ya kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024. Mapato ya Fungu hili yanakusanywa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS).

Fungu F05 limekusanya TZS 559.763 bilioni sawa na asilimia 77 ya makadirio ya kukusanya TZS 726.768 bilioni ya kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024. Mapato ya Fungu hili yanakusanywa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.

### Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango

Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, imetumia TZS 169.689 bilioni sawa na asilimia 88 ya makadirio ya TZS 193.474 bilioni. Mapato haya ya TZS 169.689 bilioni yanajumuisha Fungu F01 limetumia jumla ya TZS 27.055 bilioni sawa na asilimia 59 ya makadirio ya TZS 46.217 bilioni. Fungu F02 (Mfuko Mkuu wa Serikali) limetumia TZS 129.920 bilioni sawa na asilimia 101 ya makadirio ya TZS 128.291 bilioni. Fungu F03 (Tume ya Mipango) limetumia TZS 2.60 bilioni sawa na asilimia 42 ya makadirio ya TZS 6.157 bilioni. Fungu F04 (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali) limetumia TZS 2.137 bilioni sawa na asilimia 50 ya makadirio ya TZS 4.302 bilioni. Fungu F05 (Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali) limetumia TZS 5.71 bilioni zimetumika sawa na asilimia 98 ya makadirio ya TZS 5.837 bilioni. Fungu F06 (Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali) limetumia TZS 2.269 bilioni sawa na asilimia 85.1 ya makadirio TZS 2.667 bilioni.

### Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti za Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa kipindi cha Julai - Septemba 2023/2024

### Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ni wakala wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) inayohusika na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. ZRA ilianzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar, Sheria Nam. 11 ya Mwaka 2022.

Malengo ya ZRA ni pamoja na kuhakikisha mapato ya Serikali yanakusanywa kwa ufanisi na kwa haki pamoja na kuwahudumia wateja kwa weledi na kwa haraka.

Miongoni mwa majukumu ya ZRA ni kusimamia na kuratibu shughuli za ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuhakikisha kuna usimamizi mzuri wa sheria za kodi katika Idara na Taasisi nyengine za Serikali zinazokusanya mapato na kuishauri Serikali kuhusu masuala mbali mbali yanayohusiana na sera za fedha na kodi.

Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, ZRA imeweza kukusanya TZS 351.768 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 104.89 ya makadirio ya TZS 335.382 bilioni. Ongezeko hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa kuendelea vizuri kwa kasi ya ukuaji wa uchumi, ongezeko la wageni walioingia nchini, usimamizi imara wa ukusanyaji wa mapato hayo, kuimarika kwa huduma zinazotolewa na ZRA na kuongezeka kwa ufanisi wa watendaji wa ZRA.

Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, ZRA ilikadiria kutumia jumla ya TZS 14.28 bilioni kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo, ambapo matumizi halisi ni TZS 9.296 bilioni sawa na asilimia 71.21 ya makadirio. Kati ya fedha hizo, TZS 606 milioni zilitumika kwa kazi za maendeleo na TZS 8.689 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida.

### Changamoto Zilizobainika

ZRA inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Kuwepo kwa mwamko mdogo wa kutoa na kudai risiti.
ii. Kutokuunganishwa kwa baadhi ya hoteli za kitalii katika mfumo wa ukusanyaji mapato wa ZRA.
iii. Kuwepo kwa mwamko mdogo wa ulipaji kodi kwa hiari.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kuendelea kuimarisha ushirikiano na walipa kodi sambamba na kuongeza ufahamu wa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari.
ii. Kamati inaishauri ZRA iongeze mashirikiano na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ili kupunguza utoaji wa pesa taslimu Zanzibar. Hatua hii itasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa ukwepaji wa ulipaji kodi.
iii. Kamati inaishauri ZRA kuongeza mashirikiano na walipa kodi kwa kuandaa mabonanza ya michezo na walipa kodi, kuandaa tafrija za utoaji tuzo kwa walipa kodi bora, kuandaa makongomano, semina na mikutano kwa ajili ya kuwapa elimu wafanyabiashara ya namna ya kutelekeza wajibu wa kulipa kodi lakini pia namna ya kukuza biashara zao. Kuimarika kwa biashara za wafanyabiashara hawa zitaongeza mapato ya Serikali.
iv. Kamati inaishauri ZRA iendelee kuchukua hatua mbali mbali ili kuimarisha utendaji wake na kuwezesha huduma bora na za haraka kwa walipakodi ili kufanya mchakato mzima wa ulipaji kodi kuwa wa urahisi.
v. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba juhudi zake za kuongeza idadi ya watalii wanaokuja Zanzibar zinaenda sambamba na juhudi za kuhakikisha mapato yanayotokana na sekta ya utalii yanaongezeka kwa kuendelea na juhudi ya kuziingiza hoteli zote na mikahawa ya kitalii katika mifumo ya kidijitali.
vi. Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na mashirika yanayoratibu safari za watalii ili kukusanya taarifa kuhusu watalii wanaolipa huduma wakiwa nje ya nchi. Taarifa hizi zinaweza kutumika na ZRA ili kuhakikisha watalii wote wanalipa kodi inayostahiki.
vii. Kamati inaisisitiza ZRA kuendelea kufanya vikao na viongozi wote wa hoteli za kitalii ili kuwasisitiza umuhimu wa kutoa taarifa sahihi za wageni wanaolala katika hoteli zao. Ukiukwaji wa hatua hii, si kwamba ni vitendo vya ukwepaji kodi tu bali pia ni kuhatarisha usalama wa wageni kwani Serikali inapaswa kupewa taarifa sahihi za mahala walipo wageni wote waliyopo nchini.

## Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeundwa kwa sheria namba 11 ya mwaka 1995 na imeanza kazi rasmi kuanzia mwezi wa Julai mwaka 1996. Jukumu kubwa la TRA ni kuwa wakala wa Serikali Kuu wa kusimamia ukusanyaji wa kodi na ada mbali mbali zinazotozwa na Serikali Kuu.

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar inasimamia Kodi ya Mapato chini ya Sheria Namba 11 ya mwaka 2004 ambayo inahusu kutoza kodi ya Mapato kwa Makampuni (Corporate Tax), Kodi ya zuwio (Withholding tax), Kodi ya kutokana na faida ya kuuza rasilimali (Capital Gain), Kodi ya Mapato ya mtu binafsi (Individual Income Tax) na Kodi ya Mapato yanayotokana na ajira (PAYE). Vile vile TRA - Zanzibar inasimamia Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004, ambapo inatoza kodi za forodha kwa bidhaa zinazoingia nchini kutoka nje ya nchi. TRA - Zanzibar inakusanya kodi ya ushuru wa bidhaa chini ya Sheria ya Kodi ya Bidhaa mbali mbali pamoja na kodi ya ushuru wa bidhaa katika mafuta ya kuendeshea vyombo vya moto na VAT kwa bidhaa zinazoingia nchini.

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, TRA - Zanzibar imekusanya TZS 253.394 bilioni dhidi ya makadirio ya kukusanya TZS 253.933 bilioni hii ni sawa na ufanisi wa asilimia 99.8 ya lengo.

Katika mwezi Desemba 2023, TRA - Zanzibar ilifanikiwa kuweka rekodi kwa kukusanya kiasi cha TZS 62.941 bilioni. Hii ni rekodi mpya tangu kuanzishwa kwa ofisi hiyo, na inaonyesha mafanikio makubwa katika kukusanya mapato ya Serikali. Kamati ya Bajeti inaipongeza sana TRA -Zanzibar kwa mafanikio haya, na ni imani ya Kamati kwamba itaongeza juhudi zitakazowezesha kufanya vizuri zaidi katika utekelezaji wa majukumu yake.

### Changamoto Zilizobainika

TRA - Zanzibar inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Uchelewaji wa kutatua migogoro ya kodi katika ngazi ya Mahakama za kodi kutokana na kesi zinazotokea baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na

Walipa Kodi mbali mbali.

ii. Mwamko mdogo wa ulipaji wa kodi kwa hiari kwa wananchi.

iii. Kuongezeka kwa biashara zisizo rasmi hususan kwenye sekta ya utalii mfano 'Airbnb ni nyumba za kulalia wageni ambazo hazijasajiliwa.

iv. Ukosefu wa vituo vya huduma za ofisi za TRA ndani ya maeneo yenye mzunguko mkubwa wa kibiashara mfano kaskazini na kusini mwa Unguja.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kusimamia kwa karibu suala la utatuzi wa migogoro ya kodi katika ngazi za Mahkama za kikodi kwa kuhakikisha watendaji wanaohitajika kuwepo katika Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi wanapatikana kwa wakati ili kesi zinaposikilizwa ziweze kufikia katika maamuzi ya mwisho na kuifanya TRA na Walipa kodi kufikia kwenye maamuzi sahihi ya malalamiko yao iwapo yatajitokeza kutoka katika pande zote mbili.

ii. Kamati inaishauri TRA kuendelea kuwapa elimu wananchi kuhusiana na ulipaji wa kodi kwa hiari kwa maendeleo ya nchi yetu. Ifahamike kwamba, suala la utoaji wa elimu ni suala endelevu.

iii. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kwa kasi na hatua za ujenzi wa Bandari ya Mangapwani ili kuondosha msongamano uliopo katika bandari ya Malindi ambao unazorotesha ukusanyaji wa kodi.

iv. Kamati inaishauri TRA ikishirikiana na ZRA ije na mipango maalum ya namna ya kuyafikia maeneo ya biashara yanayoazishwa katika sekta ya utalii ikiwemo ukodishaji wa nyumba za kulala wageni pamoja na biashara nyengine kupitia sekta hiyo ili kukusanya kodi stahiki na hatimae kuongeza mapato ya TRA hiyo.

## Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)

Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni benki ya kwanza ya kibiashara iliyoanzishwa Zanzibar. PBZ inamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa asilimia 100. PBZ ina mtandao wa matawi na vituo vya huduma Zanzibar na Tanzania Bara.

Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) inachangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza uchumi wa Zanzibar kwa njia mbali mbali, ikiwa ni pamoja na Kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha, Kukuza biashara kwa kutoa mikopo kwa wafanyabiashara, Kukuza uwekezaji, Kuchangia katika maendeleo ya jamii kwa kushiriki katika shughuli mbali mbali za maendeleo ya jamii, kama vile kutoa misaada kwa mashirika yasiyo ya kiserikali na kusaidia miradi ya kijamii.

PBZ inaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha huduma zake na kuongeza mchango wake katika uchumi wa Zanzibar. Baadhi ya hatua hizi ni pamoja na Kuongeza mtandao wake wa matawi na vituo vya huduma, Kuimarisha huduma zake za kielektroniki ili kuwezesha watu binafsi na biashara kupata huduma za kifedha kwa urahisi zaidi na Kuongeza utoaji wa huduma za kifedha zinazozingatia Shariah.

Kwa upande wa mapato, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024 ilikusanya jumla ya TZS 85.980 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 26 ya kipindi kama hicho kwa mwaka 2022 ambapo mapato ya PBZ yalikuwa TZS 68.164 bilioni. PBZ imefanikiwa kuvuka malengo ya kukusanya TZS. 74.491 bilioni sawa na ongezeko asilimia 15 ya mapato halisi. Aidha, matumizi ya PBZ kwa kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024 yalikuwa TZS 46.231 bilioni. PBZ imefanikiwa kudhibiti matumizi ukilinganisha na makadirio ya kutumia TZS 49.535 bilioni kwa asilimia 7.

Taarifa zinaonesha PBZ imeendelea kufanikiwa kupata faida ya TZS 39.749 bilioni kwa kipindi cha Julai mpaka Disemba 2023, na hivyo kuvuka malengo ya kupata faida ya TZS 24.956 bilioni kwa ongezeko la asilimia 59.

### Changamoto Zilizobainika

PBZ inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Kumekuwepo na mapungufu ya matumizi ya teknolojia kama vile kutokufanya kazi mashine za ATM mara kwa mara Pamoja na kutokufanya kazi mfumo wa PBZ Mobile na kutokupatikana network jambo ambalo huzuia kufanyika miamala hata kwa mawakala wa PBZ.
ii. Kukosekana kwa ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za PBZ. Mfano, unaweka kukuta katika tawi kuna sehemu tatu za kutolea huduma za kifedha (counter) lakini kuna mhudumu mmoja (teller) tu wakati kuna foleni refu ya wateja.
iii. Kuongezeka kwa ushindani na benki nyingine za kibiashara.
iv. Kuwepo kwa huduma kwa wateja zisizoridhisha. Wateja wengi hulalamika kwa kuchukua muda mrefu sana kupatiwa huduma katika matawi na vituo vya kutolea huduma vya PBZ.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. PBZ inapaswa kuendelea kuimarisha bidhaa na huduma zake ili kukidhi mahitaji ya wateja wake. Mathalan, katika eneo hili PBZ inapaswa kuongeza mtandao wake wa matawi na vituo vya huduma, kuimarisha huduma zake za kielektroniki na kutoa huduma za kifedha zinazozingatia mahitaji ya wateja kama vile kuendelea kutoa huduma za kifedha zinazozingatia Shariah.
ii. Licha ya PBZ kukabiliwa na uhaba wa watendaji lakini inapaswa kuweka mikakati ya kuhakikisha watendaji waliyopo wanafanya kazi kwa weledi na ufanisi. Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) inaweza kuimarisha huduma kwa wateja kwa njia kadhaa, ikiwa ni pamoja na kutumia teknolojia ili kuimarisha huduma kwa wateja, Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wote wa huduma kwa wateja kuhusu namna ya kushughulikia malalamiko ya wateja kwa njia ya kirafiki na ya kusaidia, pamoja na kuweka utaratibu wa

kufuatilia malalamiko ya wateja ili kuhakikisha kuwa yanashughulikiwa kwa wakati na kwa ufanisi. Hii inaweza kusaidia PBZ kujenga uaminifu kwa wateja wake na kupunguza idadi ya malalamiko ya wateja.

iii. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za kuimarisha PBZ ili iweze kujiendesha kibiashara na hatimae kushindana na benki nyengine kama vile CRDB, NMB, NBC na benki nyengine zilizopo Tanzania.

### Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA)

Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) ni taasisi ya Serikali inayosimamia manunuzi na uondoaji wa mali za umma Zanzibar. ZPPDA ilianzishwa mwaka 2016 chini ya Sheria ya Manunuzi ya Umma Nam. 11 ya mwaka 2016.

Miongoni mwa majukumu ya Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) ni pamoja Kuandaa na kutekeleza Kanuni za manunuzi ya umma; Kusimamia na kuhakikisha manunuzi yote ya umma yanayofanywa na taasisi za umma yanazingatia kanuni za manunuzi ya umma; Kutoa mafunzo kwa watendaji wa manunuzi ya umma; Kushughulikia malalamiko yanayohusiana na manunuzi ya umma; na Kuondoa mali za umma ambazo hazihitajiki tena.

Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA) ilikadiriwa kukusanya jumla ya TZS 365 milioni na kuweza kukusanya TZS 255.06 milioni sawa na wastani wa asilimia 70 ya makadirio. Mapato hayo yametokana na ada ya usajili wa watoa huduma, ada ya mafunzo kwa wadau wa manunuzi, ada za nyaraka ya zabuni na ada ya matangazo. Aidha, Mamlaka imejipangia kutumia TZS 1.28 bilioni na kuingiziwa TZS 1.02 bilioni sawa na asilimia 79.7. Kati ya fedha hizo TZS 809.37 milioni kwa ajili ya mishahara na TZS 219.9 milioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

### Changamoto Zilizobainika

ZPPDA inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Kuwepo kwa changamoto mbali mbali katika utumiaji wa mfumo wa

manunuzi kwa baadhi ya taasisi.

ii. Kuwepo kwa changamoto ya bidhaa na huduma zinazopatikana kupitia mfumo wa manunuzi kuwa ghali zaidi kuliko bei ya soko halisi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Mamlaka ya Manunuzi iendelee kutoa mafunzo kwa taasisi za Serikali ili kuondosha changamoto katika matumizi ya mfumo wa manunuzi na hatimae kuleta ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za taasisi. Suala la utoaji wa mafunzo liwe endelevu kila inapohitajika ili lengo la kuanzishwa mfumo huu lipatikane.

ii. Kamati inaishauri Mamlaka ya Manunuzi ifanye utafiti na ije mpango madhubuti wa kukabiliana na tofauti ya bei kwa bidhaa na huduma zinazopatikana kupitia mfumo wa manunuzi kuwa ghali zaidi kuliko bei ya soko halisi.

## Shirika la Bima Zanzibar (ZIC)

Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) lilianzishwa mwezi wa Juni mwaka 1969. Shirika hili ni miongoni mwa mashirika yanayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100. Baada ya mabadiliko mbali mbali katika uendeshaji wa Mashirika ya Serikali, Shirika kwa sasa linafanya kazi zake chini ya Sheria ya Msajili wa Hazina Namba 6 ya mwaka 2021.

Miongoni mwa majukumu ya Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), ni pamoja Kusajili wanachama, Kukusanya michango ya wanachama, Kufanya uwekezaji na Kulipa Mafao kwa wanachama wake.

Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) limefanikiwa kukusanya TZS 19.5 bilioni ya mauzo ya bima ambayo ni sawa na asilimia 86 ya makadirio ya kukusanya TZS 22.6 bilioni katika kipindi cha tathmini. Aidha, Shirika limefanikiwa kupata TZS 156 milioni ya mapato yanayotokana na uwekezaji.

Kwa upande wa matumizi, katika kipindi Julai - Disemba 2023/2024 Shirika la Bima lilitumia TZS 3.9 bilioni kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa Ofisi, TZS 2.38 bilioni zimetumika kulipa madai mbali mbali ya wateja wake waliopata ajali na kutimiza matakwa ya sheria za bima, na TZS 1.7 bilioni zimetumika pia kulipa ujira kwa mawakala na madalali wanaofanya biashara ya bima kwa niaba ya Shirika.

**Changamoto Zilizobainika**

Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) linakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Baadhi ya Taasisi za Serikali Zanzibar zinashindwa kulipia malipo ya bima kwa wakati licha ya kuwahi kuchukua ankara za malipo hayo na taasisi nyengine za Serikali kutokata kabisa Bima za gari na mali za taasisi.

ii. Shirika linalazimika kuendana na miongozo mbali mbali inayotolewa kwa taasisi na Idara za Serikali jambo ambalo linalibana Shirika kuendana na uhalisia wa mahitaji ya soko la biashara za ushindani na hivyo Shirika kushindwa kukua kwa kasi.

iii. Kuwepo kwa ushindani wa kibiashara kwa Kampuni nyengine zinazotoa huduma za bima.

iv. Kiwango cha Mtaji wa Shirika kutokukidhi kupata biashara kubwa katika mfumo wa Bima Mtawanyo (Reinsurance) kunalipunguzia Shirika fursa ya kuandikisha Bima mbali mbali za miradi mikubwa iliyopitishwa katika bajeti za maendeleo za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo kulifanya Shirika kubaki na biashara kwa asilimia ndogo kutokana na mtaji mdogo uliopo.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Serikali ianze utaratibu wa kutoa mafunzo kwa watendaji wa umma kuhusu umuhimu wa kuweka bima mali za Serikali sambamba na hilo Serikali ianzishe mfumo wa ufuatiliaji wa malipo ya bima ili kuhakikisha taasisi zote

zinaziwekea mali za Serikali zinazostahiki kuwekewa bima na kuhakikisha taasisi hizo zinalipa kwa wakati.

ii. Serikali ianzishe utaratibu wa kupitia upya miongozo yake kwa mashirika yake ya kibiashara hususani yale ambayo yanafanya kazi nje ya Zanzibar. Hatua hii itasaidia mashirika kujiendesha kibiashara na kuweza kushindana na kampuni nyengine za bima.

iii. Shirika liimarishe vitengo vya utafiti na ubunifu ili kuweza kuibua bidhaa na huduma mpya zinazolingana na mahitaji ya soko.

### Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), umeanzishwa chini ya Sheria nambari 2 ya mwaka 2005, Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho katika vipindi tofauti. Lengo la Mfuko ni kuwahifadhi wanachama wake wanapopatwa na majanga ambayo husitisha au kupungua kwa kipato kutokana na sababu mbali mbali kama vile uzee, ulemavu, maradhi au kifo, pamoja na majanga mengine yaliyoainishwa katika sheria.

Miongoni mwa majukumu ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), ni pamoja Kusajili wanachama, Kukusanya michango ya wanachama, Kufanya uwekezaji na Kulipa Mafao kwa wanachama wake.

Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) umekusanya TZS 113.9 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 99.7 ya makadirio ya kukusanya TZS 114.2 bilioni.

Kwa upande wa matumizi, ZSSF imetumia jumla ya TZS 127 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 71 ya ya makadirio ya kutumia TZS 179.2 bilioni.

### Changamoto Zilizobainika

ZSSF inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Uelewa mdogo wa umuhimu wa hifadhi ya jamii kwa baadhi ya waajiri na

waajiriwa hali inayopelekea kutokuwajibika ipasavyo katika uchangiaji na usajili wa wanachama wapya.

ii. Kushuka kwa viwango vya faida katika uwekezaji wa Soko la fedha duniani hivyo kuathiri malengo ya ZSSF.

iii. Kutokuwepo na mashirikiano baina ya ZSSF, ZRA, TRA, Wakala wa Usajili wa matukio ya Kijamii Zanzibar, BPRA, ZIPA, Idara ya Uhamiaji na Kamisheni ya Utalii. Mathalan, kutokusomana kwa mifumo ya taasisi hizo hali inayopelekea kukosekana kwa taarifa sahihi za waajiri, waajiriwa na wageni wanaoingia kufanya kazi na kuondoka.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kuongeza uanachama kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa hifadhi ya jamii, kurahisisha mchakato wa uanachama, na kujenga imani katika mfuko.

ii. Kutafuta fursa za uwekezaji wenye faida na salama kwa ajili ya michango ya wanachama.

iii. Kuimarisha usimamizi wa mfuko kwa kuongeza uwazi na uwajibikaji.

iv. Kuimarisha huduma kwa wanachama kwa kurahisisha kufikia huduma, kupunguza ucheleweshaji wa malipo ya faida, na kuongeza uwazi katika shughuli za mfuko.

v. Kuimarisha mifumo ya teknolojia ya mfuko ili kuongeza ufanisi na huduma kwa wanachama.

vi. Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango iratibu vikao baina ya ZSSF, ZRA, TRA, ZCSRA, ZIPA, Uhamiaji na Kamisheni ya Utalii ili kutengeneza mpango wa pamoja wa kushirikiana na kupeana taarifa ambazo zitasaidia katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo.

# SEHEMU YA TANO
# TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA

## SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC)

Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) ni Shirika la umma linalohusika na utoaji wa huduma za utangazaji wa televisheni, redio huchangia katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. ZBC ina matawi mawili, moja Unguja na moja Pemba. Matawi haya yana vitengo mbali mbali vinavyohusiana na uzalishaji wa maudhui, usambazaji wa maudhui, na uuzaji wa matangazo.

ZBC hutoa huduma za utangazaji kwa lugha za Kiswahili, Kiarabu, na Kiingereza. Maudhui ya ZBC yanajumuisha habari, vipindi vya burudani, vipindi vya kielimu, na vipindi vya kitamaduni. ZBC ina jukumu muhimu katika kukuza utamaduni na elimu katika Zanzibar. Shirika hili linasaidia kueneza taarifa na maarifa kwa wananchi wa Zanzibar na linasaidia kuendeleza utamaduni wa Zanzibar.

Katika utekelezaji wa bajeti ZBC imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha hususan fedha za miradi ya maendeleo. Mathalan, kwa kipindi cha miezi tisa (Julai - Machi) 2021/2022, ZBC ilijipangia kutumia jumla ya TZS 14.097 bilioni na ilifanikiwa kupata TZS 482.919 milioni tu kwa ajili ya kazi za

kawaida na matumizi ya Miradi ya Maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 3. Kwa upande wa miradi ya maendeleo kulipangwa kutumika TZS 12.127 bilioni kwa ajili mradi wa uimarishaji wa matangazo ZBC na hadi kumalizika kwa mwezi wa Machi 2022 hakukuwa na fedha zilizopatikana.

**Changamoto Zilizobainika**

ZBC inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Ushindani kutoka kwa vyombo vya habari vya kibinafsi. Zanzibar ina idadi ya vyombo vya habari vya kibinafsi vinavyotoa huduma za utangazaji. Ushindani huu unapunguza mapato ya ZBC.
ii. ZBC inakabiliwa na ukosefu wa rasilimali, ikiwa ni pamoja na fedha na vifaa. Ukosefu huu wa rasilimali unaathiri uwezo wa ZBC kutoa huduma bora za utangazaji.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. ZBC inahitaji kuimarisha maudhui yake ya utangazaji kwa kuweka mipango ya kutumia teknolojia mpya, na kuimarisha kitengo chake cha biashara.
ii. Serikali inapaswa kuja na mipango madhubuti ya kuhakikisha ZBC inajiendesha kibiashara. ZBC inapaswa kuwa na watendaji wa kutosha wenye kufanya kazi kwa weledi na ufanisi, kujikita katika matumizi ya teknolojia za kisasa pamoja na kuwezesha kupatikana kwa fedha na vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya ZBC hususan uzalishaji wa vipindi, kurusha matangazo na kufuatilia matukio. Mipango hiyo iwezeshe ZBC kuweza kujitegemea na kujiendesha kibiashara na kufikia hatua ya kutoa gawio kwa Serikali badala ya kupokea ruzuku.

## KAMPUNI YA UUNGANISHAJI NA USAMBAZAJI WA MAUDHUI ZANZIBAR (ZMUX)

Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (ZMUX) ni

kampuni inayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni Nam. 15 ya mwaka 2013, na baadae kufanyiwa mapitio mwaka 2018.

Miongoni mwa majukumu ya ZMUX ni Kuanzisha na kuendeleza biashara ya maudhui katika mfumo wa kidijitali, Kuendeleza miundombinu ya upokeaji na usambazaji wa maudhui (content), Kuendeleza na kuimarisha huduma za utangazaji za ndani na nje ya nchi, na Kutekeleza majukumu mengine kama inavyoelekezwa na Sheria.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, Kampuni ilipanga kutekeleza shughuli za Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui, Kuipatia Kampuni vifaa na Huduma muhimu, Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Kampuni na Kuandaa vikao vya bodi.

Katika utekelezaji wa shughuli hizo, ZMUX ilikadiria kutumia jumla ya TZS 1,921 milioni lakini hadi kufikia Juni 30, 2023 matumizi halisi yalikuwa TZS 1,030 milioni sawa na asilimia 54. Kati ya fedha hizo zilizotumika, TZS 167 milioni ni ruzuku kutoka Serikalini kwa matumizi ya kawaida (Subvention for other charges) ambayo ni sawa na asilimia 40 ya makadirio ya TZS 421 milioni na TZS 1,525 milioni ni makusanyo ya ZMUX ambayo ni sawa na asilimia 102 ya makadirio ya kukusanya TZS 1,500 milioni.

### Changamoto Zilizobainika

ZMUX inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Kuwepo kwa ushindani mkubwa kutoka kwa watoa huduma wengine wa uunganishaji na usambazaji wa maudhui. Zanzibar kuna watoa huduma wengine wa mawasiliano, kama vile kampuni za simu za mkononi na kampuni za mtandao. Watoa huduma hawa wanatoa huduma zinazofanana na ZMUX, na hivyo kutoa shinikizo la ushindani.
ii. Uchakavu wa miundombinu, kwa kawaida vifaa vya kielektroniki huchukuwa miaka minne (4) hadi mitano (5), kwa sasa miundombinu hiyo imefikia

miaka kumi (10) jambo ambalo limepelekea kuharibika mara kwa mara na kusababisha kukosekana kwa huduma.

iii. Udogo wa ruzuku wanaopatiwa ZMUX kutoka Serikalini.
iv. Kutokana na ZMUX kutegemea wauzaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi inakumbana na changamoto ya kutumia mfumo wa manunuzi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. ZMUX iimarishe huduma zake ili kuvutia wateja zaidi kwa kuongeza chaneli za televisheni na redio za kidijitali, na kwa kuboresha ubora wa huduma zake.
ii. Ili ZMUX iweze kuimarika hatimae kuweza kujitegemea na kujiendesha kibiashara, Serikali inapaswa iweke mikakati madhubuti ya kuimarisha ZMUX kwa kuingizia fedha kwa ajili ya kuimarisha ili ifikie uwezo wa kujitegemea.
iii. Ili kukabiliana na changamoto ya ushindani wa kibiashara kutoka kwa watoa huduma wengine wa uunganishaji na usambazaji wa maudhui, Serikali inapaswa kuiwekea kanuni na miongozo rafiki ya kibiashara ili ZMUX iweze kujiendesha kibiashara na kumudu ushindani uliopo.
iv. ZMUX iratibu vikao na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA) ili kupata mafunzo na msaada wa namna taratibu za ununuzi wa bidhaa na huduma zinavyoweza katika mazingira yao. Aidha, ZMUX itapata fursa ya kuelezea changamoto zao za utumiaji wa mfumo wa manunuzi na hatimae kuweza kutafutiwa ufumbuzi wa haraka.

## MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA)

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) imeundwa chini ya Sheria ya Uwekezaji Nam. 4 ya 2018 kwa madhumuni ya kutimiza malengo ya sera ya uwekezaji vitega uchumi ya nchi na kupunguza urasimu na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka. Aidha, ZIPA inatumia Sheria mpya iliyotungwa 2023 ambayo inajuulikana kama Sheria ya Uwekezaji Zanzibar, Nam. 10 ya 2023. Jukumu kuu la Mamlaka ni kuimarisha mikakati ya kutangaza fursa za uwekezaji zitakazowavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kupata

wawekezaji wenye tija na kutoa huduma kwa wawekezaji.

### Changamoto Zilizobainika

ZIPA inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Kamati imebaini kuwa ZIPA inakabiliwa na changamoto ya upatikanaji mdogo wa fedha za maendeleo. Kwa mfano, fedha zilizopangwa kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 ni TZS 15.1 bilioni, aidha fedha iliyopatikana hadi kufikia Juni, 2023 ni TZS 4.3 bilioni sawa na asilimia 29 ya makadirio.
ii. Kamati pia ilibaini upatikanaji mdogo wa fedha za mapato kwa kodi ya mabanda, leseni na fomu za maombi kumepelekea mapato yaliyokusanywa kwa mwaka 2022/2023 kufikia asilimia 45 ambayo ni ndogo na kupelekea kuathiri matumizi ZIPA.
iii. Kuvamiwa kwa baadhi ya maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji kunarudisha nyuma jitihada za Mamlaka katika kuyaendeleza maeneo hayo. Aidha, Kamati inaishauri ZIPA kuweka alama katika mipaka ya maeneo huru ya uwekezaji.
iv. Uhaba wa fedha zinazopatikana kwa ajili ya kuendeleza maeneo huru ya uchumi.
v. Ufinyu wa Jengo la Ofisi katika kuwahudumia wateja.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kutoa kipaumbele kwa ZIPA katika fedha za maendeleo ili iweze kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuendeleza utekelezaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi pamoja na kuwezesha upatikanaji wa huduma muhimu katika maeneo huru ya uchumi.
ii. Kamati inaitaka Mamlaka kuendelea kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa maeneo ya uwekezaji nchini na kujiepusha na vitendo vya uvamizi katika maeneo ya uwekezaji. Aidha, ZIPA waweke alama katika mipaka katika maeneo yote ya uwekezaji ili kudhibiti vitendo vya uvamizi.

iii. Kwa kuwa ZIPA inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa ofisi, Kamati inaishauri kuanza kufanya upembuzi wa kina juu ya aina ya jengo ambalo litafaa kwa matumizi ya ZIPA ili mradi wa ujenzi utakapoanza uweze kuondosha changamoto zilizopo na pia kutumika kwa muda mrefu ujao.

## WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR

Wakala wa Barabara Zanzibar ilianzishwa kwa Sheria ya Wakala wa Barabara Zanzibar, Nambari 11 ya mwaka 2019. Wakala wa Barabara ina jukumu la kujenga, kutunza na kuizfanyia matengenezo barabara zote za Unguja na Pemba ili ziweze kupitika kwa usalama na kurahisisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa ufanisi zaidi.

### Changamoto Zilizobainika

Wakala wa Barabara Zanzibar inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Uchakavu na uwepo wa mashimo kwa baadhi ya njia za Unguja na Pemba. Hali hii ni kutokana na ongezeko la gari zinazobeba mizigo mizito zaidi ya uwezo wa barabara zilizopo, kukosekana kwa mitaro ya maji ya mvua hasa katika barabara za mijini kunachangia kuharibika haraka barabara hizo.

ii. Uhaba mkubwa wa vifaa vya ujenzi wa barabara ikiwemo gari ukilinganisha na kazi zilizopo kwa upande wa Unguja na Pemba.

iii. Uhaba wa wafanyakazi hasa kwenye kada za wataalamu wakiwemo mafundi wa zana na mitanbo kunarudisha nyuma jitihada za Wakala katika kufanikisha majukumu yake.

iv. Uhaba wa fedha za uendeshaji wa Ofisi na utekelezaji wa miradi kunapelekea kutokukamilika kwa majukumu ya Wakala kwa kiwango kilichokusudiwa. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 kuna miradi mingi ilishindwa kutekelezwa kwa kukosa fedha. Miongoni mwa miradi hiyo ni Mradi wa matengenezo ya barabara ya Jumbi –Tunguu, ujenzi wa barabara ya Uzini kwa Sheha Msikiti wa Ijumaa, Ujenzi wa barabara ya

Unguja Ukuu Ng'ambwa, Ujenzi wa Barabara ya Kisiwani Tumbatu, Ujenzi wa Barabara ya Micheweni Msituni na Ujenzi wa Barabara ya Mizingani Wambaa.

v. Uvamizi wa maeneo ya hifadhi ya barabara kwa ujenzi holela kunaathiri muonekano mzuri wa maeneo ya barabara zinapokamilika ujenzi wake.

vi. Wizi na uharibifu wa alama za barabarani kunaathiri watumiaji wa barabara pamoja na taswira ya barabara hasa ukizingatia kuwa alama za barabarani zinasaidia kuongoza watumiaji mbali mbali wa Barabara hizo.

vii. Uhaba na uchakavu wa majengo ya Ofisi, maabara na karakana.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kwa kuwa Serikali inaendelea na hatua za ujenzi wa barabara kwa Unguja na Pemba, Kamati inaishauri Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi katika ujenzi huo unaoendelea kuzingatia uwekaji wa mitaro ya maji ya mvua ambayo ni muhimu katika kuzifanya barabara kuweza kudumu kwa kipindi kirefu.

ii. Kamati inaishauri Wakala kuendelea na utaratibu wake wa kutenga bajeti ya ununuzi wa vifaa kwa kila mwaka na kuhakikisha kuwa, bajeti hiyo inatekelezwa ili kuondoa changamoto ya uhaba wa vifaa.

iii. Kwa kuwa Wakala inakabiliwa na uhaba wa fedha za Uendeshaji na utekelezaji wa miradi, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kuhakikisha inaipatia Wakala fedha za kutekeleza miradi iliyopangwa kwani fedha za shughuli hizi zipo kupitia vyanzo vya Mfuko wa Barabara.

iv. Kamati inaitaka Wakala kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kuyahifadhi maeneo ya barabara pamoja na kutunza alama za barabarani ili hatimae jamii iweze kuwa na uelewa wa kutunza barabara zetu pamoja na kuacha vitendo vitakavyopelekea uharibifu wa barabara hizo.

v. Kutokana na uchakavu wa majengo ya Ofisi za Wakala, maabara na karakana, Kamati inaishauri Serikali kuzipa kipaumbele taasisi ambazo

zina uhitaji mkubwa ikiwemo Wakala wa Barabara katika Mradi wa Ujenzi wa Mji wa Serikali.

## OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI (OCGS)

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar (OCGS) ni taasisi ya serikali inayohusika na kukusanya, kuchambua na kusambaza takwimu za Zanzibar. OCGS inatoa takwimu muhimu kwa ajili ya mipango ya maendeleo na sera za Serikali.
Ofisi ya Mtakwimu Mkuu inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Nam. 9 ya mwaka 2007.

Miongoni mwa majukumu ya OCGS ni:

- Kukusanya, kuchambua na kusambaza takwimu za idadi ya watu, uchumi, jamii na mazingira.
- Kufanya sensa ya watu na makazi kila baada ya miaka kumi.
- Kuandaa na kuchapisha machapisho ya takwimu.
- Kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma na sekta binafsi kuhusu takwimu.
- Kushirikiana na mashirika ya kimataifa ya takwimu.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kupitia Mpango Kabambe wa Kuendeleza Takwimu Tanzania wa Awamu ya Pili (TSMP II), Mradi wa Ujenzi wa jengo la Ofisi Mtakwimu Mkuu - Pemba.

Hatua iliyofikiwa ni utoaji wa Tunza ya Zabuni (*Notification of Award)* mzabuni aliyeshinda kuandaa michoro pamoja na usimamizi wa ujenzi kwa jengo jipya la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Pemba ambaye ni kampuni Mekon Arch Consultant Limited.

### Changamoto Zilizobainika

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Upatikanaji mdogo wa fedha za matumizi mengineyo kunarudisha nyuma utekelezaji wa majukumu ya ofisi hasa ukizingatia ofisi hii kazi zake zinaambatana na ufuatiliaji wa takwimu mbali mbali nje ya ofisi.
ii. Eneo la ujenzi wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Pemba ni dogo na hivyo inakuwa vigumu kapatikana kwa ajili ya ujenzi wa ofisi pamoja na kupata sehemu ya maegesho.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaitaka Serikali kuipatia Ofisi ya Mtakwimu bajeti ya fedha za matumizi mengineyo kama ilivyopangwa ili ofisi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.
ii. Kwa kuwa eneo la ujenzi wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Pemba lipo karibu na eneo la Wizara ya Afya, Kamati inaishauri Serikali kuipatia Wizara ya Afya eneo jengine ili iweze kuipisha Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Pemba ili mradi wa ujenzi utekelezeke kwa ufanisi.

## KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR (ZAFICO)

Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) ina jukumu la kufanya mabadiliko katika sekta ya uvuvi Zanzibar kutoka uvuvi wa kawaida na kwenda katika biashara kwa kuimarisha miundombinu ya usarifu wa samaki na dagaa, kuwawezesha wajasiriamali ili kukuza ubunifu, kuongeza thamani katika mazao ya baharini na kuchangia katika sekta ya viwanda ambavyo vitasaidia katika upatikanaji wa ajira kwa vijana kupitia uchumi wa buluu.

## Changamoto Zilizobainika

ZAFICO inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Katika eneo la mradi wa wajasiriamali wa kusarifu dagaa KAMA, baadhi ya maeneo ya kiwanda, kumebainika mmong'onyoko wa ardhi hali inayohitaji mazingatio ya mapema.

ii. Sehemu iliyotengwa kupokelea dagaa ni dogo katika eneo la KAMA, kutokana na sehemu iliyobakia kumilikiwa na watu binafsi.
iii. Ukosefu wa usafiri kwa ZAFICO unakwamisha ufuatiliaji wa kazi ikiwemo biashara ya samaki.
iv. Ukosefu wa fedha unakwamisha utekelezaji wa shughuli za Kampuni.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali ije na mipango Madhubuti ya kuiwezesha ZAFICO kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ili iweze kujiendesha kibiashara na hatimae iweze kutoa gawio kwa Serikali badala kupokea ruzuku. Aidha, tunapaswa kuimarisha ZAFICO kwa sababu ni taasisi ina nafasi kubwa ya kutoa mchango mkubwa katika Sekta ya Uchumi wa Buluu
ii. Kwa kuzingatia umuhimu wa kiwanda cha KAMA katika kusarifu dagaa, Kamati inasisitiza kuwekwe mazingatio maalum ya kukabiliana na hali ya mmong'onyoko wa ardhi katika eneo hilo.

## SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR (ZHC)

Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC) limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Nambari 6 ya mwaka 2014 ambalo limepewa majukumu ya kuwapatia wananchi makaazi bora na salama pamoja na kuongeza Pato la Taifa.

Kwa mwaka fedha 2022/2023, Shirika la Nyumba lilipanga kukusanya jumla ya TZS 9.903 bilioni kutika katika vyanzo vyake tofauti. Hadi kufikia mwezi Juni 2023, Shirika lilikusanya jumla ya TZS 4.529 bilioni sawa na asilimia 45.7. Kwa upande wa matumizi ya Shirika la Nyumba, hadi kufikia Juni 30, 2023 limefanikiwa kutumia jumla ya TZS 4.497 bilioni sawa na asilimia 50.5 ya makadirio ya TZS 8.898 bilioni.

**Changamoto Zilizobainika**

Shirika la Nyumba Zanzibar inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Kamati imebaini nyumba nyingi zinazomilikiwa na Shirika la Nyumba kuwa ni chakavu kutokana na kutokufanyiwa matengenezo muda mrefu.

ii. Kodi ndogo zinatolewa na wapangaji katika nyumba za maendeleo hazikidhi haja, hali ambayo inapelekea Shirika kushindwa kufanya matengenezo kwa kiwango kinachotakiwa.

iii. Shirika linakabiliwa na wadaiwa sugu.

iv. Shirika kushindwa kukopa katika taasisi za kifedha kutokana na kiwango kikubwa cha riba.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kuliwezesha Shirika la Nyumba kuchukua hatua za haraka za kukabiliana na wadaiwa sugu kwa mujibu wa Sheria iliyoanzishwa ili kuliwezesha Shirika kupata mapato yake na kuweza kujiendesha.

ii. Kamati inalishauri Shirika kuongeza kiwango cha kodi kwa nyumba zake kwa lengo la kuliwezesha Shirika kuongeza mapato ambayo yataweza kutumika kufanya matengenezo ya nyumba za Shirika.

iii. Kamati inalishauri Shirika kutafuta wawekezaji ili kufanya matengenezo pamoja na ujenzi wa nyumba mpya.

## SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC)

Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar ambalo linabeba historia kubwa ya maendeleo ya uchumi Zanzibar kupitia uuzaji wa Karafuu.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika lilipanga kukusanya jumla ya TZS 33.8 bilioni kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali ikiwemo mauzo ya karafuu, mauzo ya mafuta ya mimea, mapato yatokanayo na majengo, mauzo ya Tawi la ZSTC lililopo Dar es Salaam pamoja na mauzo yatokanayo na bidhaa za viungo. Mapato halisi ya Shirika yamefikia TZS 13.9 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 41 ya makadirio. Na kwa upande wa matumizi kwa kipindi cha robo ya kwanza, Shirika lilikadiria kutumia TZS 31.4 bilioni kwa ajili ya uendeshaji ambapo matumizi halisi yalifikia TZS 20.1 bilioni sawa na asilimia 65 ya makadirio kwa kipindi cha tathmini.

### Changamoto Zilizobainika

ZSTC inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Kuwepo kwa uwelewa mdogo wa madaraja kwa wakulima wa karafuu kwa kuhisi wanadhulumiwa kwa kupewa madaraja ambayo hawastahiki kupata kwa mujibu wa karafuu walizozipeleka.

ii. Uhaba wa rasilimali watu katika Shirika kumepelekea kulibebesha mzigo Shirika kwa kuajiri wafanyakazi wa mkataba wakati wa msimu wa mavuno.

iii. Changamoto nyengine ambayo linalikabili Shirika ni bakaa ya mafuta yatokanayo na mimea ambayo imetokana na bei iliyopo kwa sasa katika soko kutokuendana na gharama za uzalishaji.

iv. Uchache wa manunuzi ya zao la karafuu kwa wakulima kutokana na msimu mdogo wa uzalishaji kumepelekea Shirika kuuza kiasi kidogo cha karafuu ukilinganisha na vipindi vyengine.

v. Kuendelea kuwepo kwa vitendo vya usafirishaji wa karafuu kwa njia ya magesho kunalipelekea Shirika kuchukua nguvu ya ziada kukabiliana na hali hiyo.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri ZSTC kutumia teknolojia ya kisasa ili kuweza kutambua madaraja ya karafuu, hatua ambayo itaepusha malalamiko kwa wakulima.

ii. Kamati inaishauri Serikali kuangalia vyema uhitaji wa rasilimali watu katika baadhi ya taasisi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao

iii. Kamati inaishauri Shirika kutafuta bidhaa mbadala ambazo zitaweza kuliongezea mapato Shirika kipindi cha msimu mdogo wa zao la karafuu.

iv. Kamati inaishauri Serikali kupitia Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuendelea kushirikiana na ZSTC ili kuchukua hatua za pamoja za kukabiliana magendo ya karafuu. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kuipatia KMKM mafuta ya kutosha kwa ajili ya kuwawezesha kufanya doria kwa ufanisi.

### WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR (ZBA)

Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) ilianzishwa kupitia Tangazo la Kisheria Nam. 50 ya mwaka 2017 ikiwa na malengo ya kutoa ushauri elekezi katika kusanifu na kusimamia miradi ya ujenzi wa majengo pamoja na usimamizi wa nyumba za Serikali pamoja na kujenga, kukarabati majengo na miundombinu inayohusiana na ujenzi wa majengo ya Serikali.

Kwa kipindi cha Julai – Disemba 2023, Wakala ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 181.8 milioni kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali ikiwemo kodi za majengo, kazi za biashara pamoja na ushauri elekezi. Hadi kufikia Disemba 2023, Wakala imeweza kukusanya jumla ya TZS 1,986,500 sawa na asilimia 1.09 ya makadirio. Sababu kuu ya mapungufu hayo ni kutokana na kuhama kwa hesabu za mapato hayo kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi na kuhamishiwa hesabu katika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

## Changamoto Zilizobainika

ZBA inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Kutokana na kutokuwa na Fungu (Vote), ZBA inakabiliwa na changamoto ya uwepo ugumu katika upatikanaji wa fedha na ukusanyaji wa mapato, hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli zake ambazo mara nyingi zinahitaji watendaji kutoka nje ya ofisi na Kwenda maeneo ya miradi.

ii. ZBA inakabiliwa na uhaba wa watendaji (wataalamu).

iii. Kuwepo kwa upungufu wa vitendea kazi kunakopelekea kutokutimiza majukumu kwa ufanisi.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kutokana na umuhimu na upekee wa ZBA katika kusimamia miradi ya ujenzi, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango kuipatia ZBA Fungu (Vote) ili kurahisisha upatikanaji wa fedha na ukusanyaji wa mapato. Hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa shughuli za ZBA.

ii. Kamati inaishauri Serikali kuja na mipango madhubuti ambayo itaisaidia ZBA kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwezeshwa kupata watendaji wenye weledi pamoja na nyenzo za kufanyia kazi.

## WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR (ZEEA)

Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar imeanzishwa kwa Sheria Nam. 2 ya mwaka 2022 ikiwa na malengo mbali mbali ikiwemo kuimarisha mazingira wezeshi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuongeza tija, uzalishaji, ufanisi na masoko ya bidhaa za wajasiriamali na wafanyabiashara nchini.

Mbali na hayo Wakala pia inajihusisha na kuwaunganisha wajasiriamali na wafanyabiashara na vituo vya mafunzo ya amali.

### Changamoto Zilizobainika

Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Wakala inakabiliwa na uhaba wa rasilimali watu

ii. Kutokuwasilishwa kwa wakati kwa asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya Mfuko wa makundi maalum

iii. Kutokuwepo na kanuni/Sheria ya kuwashitaki wadaiwa sugu katika mfuko wa uwezeshaji.

iv. Wakala kutokuwa na jengo la Ofisi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Afisi ya Rais – Kazi, Uchumi na Uwekezaji wakati wa utungaji wa Kanuni, ni vyema kuzishirikisha na benki ambazo zinatoa mikopo ili kuweka masharti ambayo yatamuwezesha wananchi kurudisha mikopo hiyo kwa wakati.

ii. Kwa vile mapato ya Serikali za Mitaa yanaingia moja kwa moja katika Mfuko Mkuu, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango kuwasilisha moja kwa moja asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa kwa Mfuko wa makundi maalum.

iii. Kamati inaitaka Wakala kufanya mapitio kwa wajasiriamali wote waliopatiwa mafunzo ili kuweza kupata taarifa sahihi za wajasiriamali

ambao wamekidhi vigezo vya kupata Alama ya Ubora.

iv. Kamati inaishauri Wakala kuendelea na utoaji wa elimu kwa wajasiriamali wakati wa utoaji wa mikopo na namna bora ya kuitumia mikopo hiyo katika uzalishaji.

v. Kamati inaishauri Serikali kuwapatia jengo Wakala wa Uwezeshaji ili watendaji waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)

Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) limeanzishwa chini ya Sheria ya Shirika la Umeme Zanzibar, Sheria Nam. 3, mwaka ya 2006. Miongoni mwa majukumu makuu ya ZECO ni pamoja na kuwezesha uzalishaji, usafirishaji, usambazaji na uuzaji wa umeme Zanzibar.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, ZECO imekusanya jumla ya TZS 168.19 bilioni sawa na asilimia 95.95 ya makadirio ya kukusanya TZS 175.29 bilioni. Makusanyo hayo yametokana na mauzo ya umeme shilingi 159.08 bilioni na TZS 9.10 bilioni ni mapato mengineyo. Kwa upande wa matumizi, Shirika la Umeme limetumia jumla ya TZS 167.97 bilioni ambapo sawa na asilimia 96 ya makadirio yaliyowekwa ya jumla ya TZS 174.52 bilioni.

### Changamoto Zilizobainika

ZECO inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya umeme mdogo kwa baadhi ya maeneo ya Zanzibar na vilevile kuna ongezeko la matumizi ya umeme kwa wananchi wa kawaida na wawekezaji.

ii. Kuwepo kwa baadhi ya taasisi za Serikali kushindwa kulipa madeni ya umeme kwa muda mrefu. Madeni hayo, yamefikia TZS 60.64 bilioni.

iii. Kuwepo kwa uvamizi katika njia kuu za usambazaji umeme “buffer zone”

kama vile ujenzi au ufanyaji wa biashara.

iv. Kuwepo kwa uharibifu wa Miundombinu ya usambazaji wa umeme kutokana na uchimbaji wa mchanga kwenye njia kuu za umeme na wizi wa nyaya za umeme. Vilevile kuna baadhi ya wateja wasiokua waaminifu kutumia umeme kinyume na utaratibu na kulikosesha Shirika mapato.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kuja na mpango wa kuitatua changamoto ya baadhi ya taasisi za Serikali kushindwa kulipa madeni yao kwa ZECO. Changamoto hii ni ya muda mrefu, hivyo inahitaji ufumbuzi wa haraka.

ii. Kamati inaishauri Serikali, Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Shirika la Umeme kuanza kufanya tafiti za kupata vyanzo vyengine vya umeme.

## SHIRIKA LA BANDARI (ZPC)

Shirika la Bandari limeanzishwa rasmi mwezi Julai 1977 chini ya Sheria Namba. 1 ya mwaka 1997 na lina jukumu la kuziendesha, kuzisimamia na kuziendeleza Bandari. Kazi za msingi za Shirika ni kutoa huduma za uingiaji na utoaji wa meli Bandarini, ufungaji na ufunguaji wa meli hizo gatini, uangalizi wa alama za kuongozea usafiri wa bahari unaojumuisha minara na maboya, usimamizi wa vyombo vya usafiri wa bahari kwenye maeneo ya Bandari kwa upande wa mizigo na shehena nyenginezo. Pia, Shirika lina wajibu wa kuhudumia mizigo kwa kazi ya upakizi, uteremshaji na kuhifadhi katika bandari zake.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Shirika la Bandari Pemba lilikadiria kukusanya jumla ya TZS 2.7 bilioni kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato, hadi kufikia Juni 30, 2023 jumla ya shilingi 2.1 bilioni zimekusanywa sawa na asilimia 75 ya makadirio. Aidha, Shirika la Bandari Pemba lilipanga kutumia jumla ya TZS 1.6 bilioni na hadi kufikia 30 Juni, 2023 jumla ya TZS 1.2 bilioni zimetumika sawa na

asilimia 80 ya makadirio.

### Changamoto Zilizobainika

Shirika la Bandari linakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Uchakavu wa magari ya ofisi kunalipelekea Shirika kupata hasara ya matengenezo ya kila siku na kunapelekea ugumu wa kazi za ufuatiliaji.
ii. Kukosekana kwa mifumo ya kisasa ambayo husaidia kufanya shughuli za bandari kwa ufanisi.
iii. Uhaba wa wafanyakazi, vitendea kazi na majengo ambapo hupunguza kufanya kazi zake kwa wakati pamoja na kwa ufanisi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kwa kuwa suala la vitendea kazi ikiwemo vifaa vya kuendesha ofisi na usafiri vinahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kila siku za Shirika, Kamati inaishauri Shirika kuendelea kufuatilia upatikanaji wake kupitia bajeti zao ili kazi za Shirika ziweze kufanyika kwa ufanisi ikiwemo shughuli za ufuatiliaji.

ii. Kamati inashauri Shirika la Bandari kuhakikisha mfumo wa e-Port unatekelezwa kwa ufanisi na uweledi mkubwa ili kuondokana na changamoto ya kutofikia malengo kwenye utekelezaji wa majukumu.

## MTHAMINI MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imeanzishwa kwa Sheria ya Usajili wa Wathamini namba 5 ya mwaka 2015 kwa dhumuni la kuhakikisha usimamizi mzuri wa uthaminishaji rasilimali kwa malengo mbali mbali ya sekta ya Umma, biashara na wananchi kwa ujumla. Katika kipindi cha Julai - Disemba, 2023/2024, Ofisi ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 160 milioni kutoka Ada ya uthamini inayotokana na uthibitishaji wa ripoti za uthamini (approval fee). Jumla ya TZS 38. 03 milioni zimekusanywa sawa na asilimia 24%. Kwa upande wa matumizi, fedha zilizopangwa ilikuwa ni jumla ya TZS 111.5 milioni ikiwa ni fedha za ruzuku

kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Disemba, 2023 jumla ya TZS 51.7 milioni zimepatikana sawa na asilimia 50 ya makadirio.

### Changamoto Zilizobainika

Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Kushuka kwa mapato ya ofisi kutokana na kazi nyingi zinazoletwa na taasisi za Serikali kutokulipiwa ada ya uthamini.

ii. Kukosekana kwa mifumo ya kisasa (kidigitali) kuhifadhia ripoti za uthamini.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kwa kuwa Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali Zanzibar inategemea ada ya uthamini kuwa ndio chanzo chake cha Mapato, Kamati inaishauri Serikali kusimamia taasisi zake kulipia ada ya uthamini pindi wanapofanyiwa kazi zao ili kuifanya ofisi kukusanya mapato yake kutokana na kazi wanazozifanya.

ii. Kwa kuzingatia umuhimu wa mifumo ya kidigitali katika kuhifadhia taarifa, Kamati inaitaka Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali Zanzibar kujipanga kuwa na mifumo ya kidigitali ambayo itatumika katika kuhifadhia taarifa za tathmini.

# SEHEMU YA SITA

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA PROGRAMU MBALI MBALI

### MRADI WA ELIMU YA JUU KWA MABADILIKO YA KIUCHUMI (HEET) ZANZIBAR

Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET) unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) kupitia mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia (WB) ambao una thamani ya Dola za Marekani milioni 425 sawa na TZS 972 bilioni. Mradi wa HEET una lengo la kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kujenga muunganiko imara kati ya elimu ya juu na soko la ajira. Hatua hii inaweza kufikiwa kwa kuwapatia wanafunzi ujuzi unaoendana na soko la ajira. Mradi huu ambao umeanza kutekelezwa mwaka 2023, unatarajiwa kukamilika mwaka 2027.

Kwa upande wa Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ndio kilichonufaika na mradi huu, kikiwa ni moja katika vyuo vikuu 14 vya Tanzania na ni taasisi pekee kwa Zanzibar iliyobahatika kunufaika na fedha za utekelezaji wa Mradi wa HEET, kimetengewa jumla ya Dola za Marekani milioni 20 sawa na TZS 45.9 bilioni.

SUZA imepanga kutekeleza mradi huu katika maeneo makuu saba (7) ya vipaumbele ambayo ni: Ujenzi au ukarabati wa miundombinu, Uimarishaji wa mitaala na kuanzisha mbinu bora za ufundishaji, Kuimarisha matumizi ya tafiti na uwezo wa ubunifu, Kujenga uhusiano wa kiutendaji na sekta binafsi, Kuimarisha matumizi ya teknolojia za kidijitali katika kufundisha na kujifunza, Kukuza uwezo wa kujitegemea kimapato pamoja na Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa kitaaluma na Uongozi wa SUZA.

#### Changamoto Zilizobainika

Katika utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET), SUZA inakabiliwa na changamoto mbali mbali, ikiwa ni pamoja na:

i. Uhaba wa fedha za kuwezesha kutekeleza kwa baadhi ya kazi za mradi na kukosekana kwa maposho ya watendaji wa mradi.
ii. Ujuzi mdogo wa watendaji juu ya utekelezaji wa shughuli za mradi mikubwa ya Benki ya Dunia (WB).
iii. Taratibu za manunuzi zinachelewesha hatua za ununuzi wa bidhaa na huduma hali inayopelekea kupunguza kasi ya utekelezaji wa mradi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ishirikiane na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, kupitia bajeti ya SUZA 2024/2025 itenge kiasi maalum cha fedha kwa ajili ya posho za watendaji wanaotekeleza mradi huu ili kuwawezesha kutekeleza mradi huu kwa ufanisi.
ii. Kamati inaishauri SUZA kuomba msaada kwa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ajili ya kupewa mafunzo maalum na mbinu ya namna ya kutekeleza miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB). Benki ya Dunia (WB) imekuwa ikitekeleza mara kwa mara miradi ya namna hii, kwa hiyo wana uzoefu wa kutosha.
iii. Kamati inaishauri SUZA ufanye mawasiliano na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA) ili kuratibu kikao cha kupata mafunzo na msaada wa namna taratibu za ununuzi wa bidhaa na huduma zinavyoweza kufanyika katika hali ya kawaida na wakati wa dharura.

## MRADI WA UJENZI WA MASOKO YA MWANAKWEREKWE, JUMBI NA CHUINI

Mradi wa Ujenzi wa Masoko unatekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Katika kufanikisha utekezaji wa Mradi huu, Afisi ya Rais iliunda Kamati ya Wataalamu kutoka taasisi mbali mbali za Serikali kwa ajili ya kufanya makadirio ya gharama za ujenzi wa masoko yote ambayo utekelezaji wake unalenga kuwainua wajasiriamali kwa kuwapa fursa ya kuwa na maeneo maalum ya

kufanya biashara zao.

Katika makisio yaliyofanywa awali ya mradi huu kwa soko la Chuini gharama zake zilikuwa TZS 32.071 bilioni, Mwanakwerekwe TZS 29.890 bilioni na Jumbi ni TZS 12.850 bilioni. Kutokana na mapungufu yaliyobainika ikiwemo baadhi ya kazi kutoingizwa kwenye nyaraka za ujenzi, mchoro wa soko la Jumbi kutoendana na eneo la ujenzi, kutokukamilika kwa michoro ya huduma hali iliyopelekea Wakala wa Majengo ambao ndio wasimamizi wa ujenzi wa masoko yote matatu kupitia michoro yote na kuandaa gharama halisi za ujenzi na kupelekea kuwepo kwa mabadiliko ya gharama za kila soko ambapo kwa soko la Chuini gharama mpya zilifikia TZS 42.575 bilioni, soko la Mwanakwerekwe TZS 35.586 bilioni na Soko la Jumbi ni TZS 24.252 bilioni. Jumla ya gharama zilizokisiwa awali zilikuwa TZS 74318 bilioni na gharama mpya zilifikia TZS 102.412 bilioni.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuongezeka kwa gharama za ujenzi wa masoko yote matatu kutokana na kutofautiana kwa makisio ya awali yaliyofanywa na Ofisi ya Idara Maalum za SMZ pamoja na kuongezeka kwa kazi katika masoko yote.
ii. Mradi wa ujenzi wa masoko ni mkubwa sana kuwahi kufanyika hapa Zanzibar hivyo kumekuwa na mabadiliko mbali mbali kadiri ujenzi unavyoendelea.
iii. Mradi huu haukuwekewa bajeti kwenye Wizara lakini fedha zake zimeingizwa Wizarani (Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ) hali inayopelekea Wizara kufanya matumizi kwa baadhi ya mafungu yake na baadhi ya wakati inabidi kuomba bajeti ya ziada ili kupata fungu la matumizi.
iv. Baadhi ya maeneo ya utekelezaji wa mradi yanakabiliwa na changamoto za kimazingira ikiwemo soko la Jumbi ambalo lilikuwa na taka nyingi, aidha soko la Chuini ardhi yake ina maji ambayo yanahitaji kuangaliwa kwa karibu wakati ujenzi unaendelea ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza baadae.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Licha ya kubainika kwa changamoto za ongezeko la gharama katika utekelezaji wa mradi, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada ya kuendeleza ujenzi wa masoko ambayo yatawapata fursa wajasiriamali kuwa na maeneo maalum katika utekelezaji wa shughuli zao.
ii. Kwa kuwa mradi huu utekelezaji wake unasimamiwa na Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inaipatia Afisi hii fedha za mradi kwa wakati kwa ajili ya kukamilisha shughuli zake zilizopangwa.
iii. Kamati inaitaka Serikali kusimamia kwa karibu utekelezaji wa mradi huu ikiwa ni pamoja na kutafuta ufumbuzi wa kudumu kwa changamoto za kimazingira zinazojitokeza kwa eneo la Jumbi na Chuini.

## MRADI WA UIMARISHAJI WA MIUNDOMBINU YA SKULI

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) inatekeleza Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Skuli ambao lengo lake ni kuimarisha miundombinu na kuweka mazingira mazuri ya kufundishia, kujifunzia kwa ajili ya kutoa elimu bora na kuongeza ufaulu wa wanafunzi hasa wa masomo ya sayansi.

Katika Kipindi cha Oktoba – Disemba, 2023, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya madarasa 325, ujenzi wa dakhalia, ukarabati wa Skuli na Ujenzi wa Ofisi ya Elimu za Wilaya. Jumla ya TZS 59.874 bilioni zimepangwa kutumika katika kukamilisha miundombinu hiyo.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuwepo kwa bajeti ndogo katika Sekta ya Elimu ukilinganisha na mahitaji ya kuimarisha miundombinu ya elimu. Katika kuimarisha miundombinu ya elimu, Serikali inalenga kufikia shabaha ya wanafunzi 45 kwa darasa kwa mkondo mmoja wa skuli kutoka wastani wa wanafunzi 62 kwa darasa.
ii. Kuongezeka kwa gharama za kuendesha na kutunza majengo ya kisasa.

Wizara ya Elimu katika kuimarisha miundombinu ya elimu inafanya ujenzi wa skuli za ghorofa, ujenzi wa dakhalia hali inayopelekea kuongezeka kwa gharama za kuyaendesha majengo hayo ikiwemo gharama za umeme pamoja na utunzaji wa majengo.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaipongeza Wizara kwa jitihada ya kusimamia utekelezaji wa uimarishaji wa miundombinu ya Skuli. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti katika sekta ya elimu ili malengo ya kuimarisha miundombinu ya elimu nchini yaweze kufikiwa kwa kiwango kinachokusudiwa.

### MRADI WA UJENZI WA MAHKAMA ZA MIKOA

Mahkama ya Zanzibar imepanga kuimarisha utoaji wa huduma kwa ujenzi na ukarabati wa majengo yake ili kupunguza misongamano na kuwezesha mazingira rafiki katika utoaji huduma za Mahkama na kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mahkama ya Zanzibar imeidhinishiwa jumla ya TZS 25 bilioni kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya Mahkama za Mikoa na Wilaya.

Gharama zinazotarajiwa kutumika katika ujenzi huo kwa upande wa Pemba ni TZS 14 bilioni. Ujenzi umepangwa kujengwa na Mkandarasi kutoka kikosi cha JKU. Aidha, katika utekelezaji wa ujenzi kwa upande Unguja Mjenzi ni Kampuni ya CRJE East Africa LTD na gharama zinazotarajiwa kutumika ni TZS 28,839 bilioni.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuchelewa kuanza kwa shughuli za ujenzi wa Jengo la Mahkama ya Konde Wilaya ya Micheweni kutokana na kulazimika kuondolewa kwa jengo la zamani lilokuwa chakavu ili kupisha ujenzi wa jengo jipya.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Afisi ya Mahkama Zanzibar kuhakikisha inasimamia vizuri

kwa kila hatua za utekelezaji wa mradi ili ujenzi ufanyike kwa kiwango bora.

## MRADI WA UKARABATI WA MAGHALA NA UHIFADHI WA CHAKULA

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imetengewa jumla ya TZS 22.5 bilioni kwa ajili ya Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Uhifadhi wa Chakula (Development of Strategic Food Reserve Infrastructure Project in Zanzibar). Lengo la utekelezaji wa Mradi huu ni kuwepo kwa upatikanaji wa usalama wa uhifadhi na uhakika wa upatikanaji wa chakula kwa asilimia 65. Miongoni mwa shughuli zinazotarajiwa kufanywa ni pamoja na ukarabati wa maghala Matano Unguja 3 na Pemba 2.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kukosekana maeneo ya kutosha ya kuhifadhia chakula ambapo kwa sasa Wizara ina maghala 13 ambapo matatu yanatumika kuhifadhia chakula cha akiba yenye uwezo wa tani 3,100, maghala 5 yanatumika kuhifadhia mbolea na maghala 5 yanatumika kuhifadhia mbegu.
ii. Kutokana na kukosa kwa maghala ya kutosha ya kuhifadhia chakula inapelekea kuwepo kwa athari ya kutojitosheleza kwa chakula katika nchi, kutokuwepo kwa uhakika wa chakula wakati wa dharura na Mfumko wa bei za vyakula nchini kunakoathiri wananchi hasa wa kipato cha chini.
iii. Uhaba wa fedha za OC zinapelekea ugumu wa kuendesha kazi za mradi.
iv. Kuchukua muda mrefu kwa mchakato wa manunuzi hali inayopelekea kutokupatikana kwa fedha za mradi kwa wakati.
v. Uhaba wa vitendea kazi ikiwemo mafuta kunapelekea ucheleweshaji wa kazi hasa za ufuatiliaji wa nje ya ofisi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Katika utekelezaji wa Mradi wa Ukarabati wa Maghala, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kukamilisha taratibu zinazohitajika ikiwemo za manunuzi

ili waweze kupatiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

ii. Kamati inaitaka Wizara kuwa makini katika usimamizi wa mradi wa ukarabati wa maghala kwa kuzingatia ubora wa matengenezo yanayofanyika pamoja na kufanya ufuatiliaji wa hatua mbali mbali za matengenezo ili maghala hayo yafikie katika ubora unaohitajika.

## MRADI WA UANZISHWAJI WA KITUO CHA KUHIFADHIA DATA ZA MAFUTA NA GESI ASILIA

Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA) imeanzishwa mwaka 2017 chini ya Kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia Nam. 6 ya mwaka 2016. Jukumu kuu la Mamlaka hii ni kusimamia na kudhibiti shughuli zote za utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar ambazo utekelezaji wake unafanywa kupitia Programu kuu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu. Mamlaka inasimamia uanzishwaji wa kituo cha kuhifadhia Taarifa (Data) za Mafuta na Gesi Asilia kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 81(4) cha Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia Nam.6 ya mwaka 2016.

Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Data za Mafuta na Gesi Asilia umepangwa kwa muda wa miaka mitatu (3), kuanzia mwaka wa fedha wa 2022/2023 hadi 2024/2025. Gharama za mradi zinakisiwa kufikia jumla ya TZS 46 bilioni. Mradi utahusisha ujenzi wa kituo cha Muda cha Kuhifadhia Taarifa (Temporary Data Center) katika Ofisi za Mamlaka, Ujenzi wa Jengo la Kudumu la Kuhifadhia Data, Ujenzi wa Miundombinu ya TEHAMA pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wa Mamlaka katika maeneo maalum ya Usimamizi wa Data za Mafuta Na Gesi Asilia.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kwa kipindi cha Julai Disemba, 2023 hakukuwa na fedha za Mradi zilizopatikana, ambapo kwa kipindi hicho Jumla ya TZS 2.5 bilioni

zilipangwa kutumika kati ya TZS 4 bilioni zilizopangwa kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

ii. ZPRA inategemea ruzuku pekee kutoka Serikalini na hawana vyanzo vyengine vya mapato.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kwa kuwa Kamati imeelezwa kuwa, maandalizi ya ujenzi wa chumba cha kuhifadhia Taarifa (Data) za Mafuta na Gesi cha kudumu yanaendelea kufanyika, Kamati inaishauri Serikali kuipa ZPRA kipaumbele kwa kuipatia fedha za kuendeleza ujenzi huo kwa wakati kwani kukamilika kwake kutainufaisha sana Zanzibar.

ii. Kamati inaishauri Mamlaka kuendeleza mashirikiano na taasisi za ndani na za nje ambazo zinazofanana utendaji wa majukumu yako ili kuweza kuongeza ujuzi hasa katika utumiaji wa "software" katika kusoma taarifa za mafuta na gesi asilimia na namna ya kuzitunza taarifa hizo.

**MRADI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI MAJI ZANZIBAR**

Kamati ya Bajeti katika muendelezo wa kazi zake ilipokea taarifa ya Programu ya Umwagiliaji Maji Zanzibar kwa lengo la kufahamu hatua zilizofikia za utekelezaji wa mradi huo na mambo mengine yanayohusiana na utekelezaji wa mradi.

Programu ya Umwagiliaji Maji inahusisha ujengaji wa misingi ya umwagiliaji katika mabonde 6 maeneo tofauti. Mabonde hayo ni Kinyasini lenye ukubwa wa hekta 184, eneo la Chaani hekta 71, eneo la Kibokwa hekta 147, eneo la Kilombero hekta 292, eneo la Mlemele hekta 44 pamoja na eneo la Cheju lenye ukubwa wa hekta 314. Misingi ya saruji yenye urefu wa kilomita 47.74, misingi ya udongo yenye urefu wa kilomita 47.82, misingi ya kutolea maji mashambani yenye urefu wa kilomita 72.6 pamoja na barabara za mashambani za kifusi zenye

urefu wa kilomita 36.1. Programu hii pia inahusisha ujengaji wa mabwawa matatu katika maeneo tofauti. Bwawa la Kinyasini, bwawa la Chaani pamoja na Bwawa la Mlemele. Pia inahusisha uchimbaji wa visima 35, ambapo kwa bwawa la Cheju kulichimbwa visima 14, Kilombero visima 15 na Kibokwa visima 6.

### Changamoto Zilizobainika

i. Baadhi ya maeneo ya bwawa la Chaani kuna uvujaji wa maji (leakage), hali hii ambayo imesababisha kuanzwa taratibu za ulazwaji wa mpira wa plastiki (water proofsheet with geotextile membrane) ambao utazuia uvujaji wa maji.

ii. Kukosekana kwa fedha za malipo ya awali kwa mkandarasi hali ambayo imepelekea kuzorota kwa utekelezaji wa mradi.

iii. Kukosekana kwa fedha za kuwalipa wataalamu wanaosimamia mradi na kupelekea Wizara kutumia fedha za matumizi mengine (other charges) ili kuwalipa wataalamu hao.

iv. Kutokana kwa wakati wahusika wa ufungaji wa mita katika bwawa la Chaani.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali katika hatua za awali katika utekelezaji wa miradi kufanya upembuzi yakinifu wa ili kubaini athari ambazo zinaweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi ili kuepuka gharama za ziada.

ii. Kamati inaishauri Wizara kuwa makini katika kuangalia utekelezaji wa miradi na gharama zinazotumika hasa katika kipindi ambacho miradi hiyo hukabiliana na marekebisho mbali mbali.

iii. Kamati inazitaka Taasisi zote ambazo zinahusika katika utekelezaji wa miradi kuwa na mashirikiano ya karibu ili uweze kutekelezwa kwa ufanisi.

## MRADI WA UHUISHAJI NA UIMARISHAJI WA MFUMO WA USAMBAZAJI MAJI ZANZIBAR

Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar umeanzishwa kwa lengo la mradi huu ni kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi, salama na ya kutosha kwa gharama nafuu kwa watu pamoja na sekta kwa kutumia teknolojia za usimamizi wa rasilimali maji zenye kuzingatia utunzaji wa mazingira ambao utahusisha uchimbaji wa visima 64, ulazaji wa mabomba ya uzalishaji na usambazaji majikwa urefu wa kilomita 466.9, ufungaji wa mita (House connections) pamoja na ujenzi wa matangi 15 yenye ujazo tofauti. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya India kupitia benki ya Exim ya India na utagharimu jumla ya Dola za Kimarekani milioni 92.18. Hadi kufikia Julai 2023, utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 67 ya makadirio ya fedha zote.

### Changamoto Zilizobainika

i. Ufinyu wa nafasi katika Bandari ya Zanzibar na msongamano wa meli za mizigo kunapelekea uchelewaji wa utoaji wa vifaa hali ambayo imesababisha kuongezeka kwa muda wa ukamilikaji wa mradi.

ii. Kuwepo uchelewaji wa malipo ya wakandarasi kutokana na taratibu za kibenki.

iii. Kamati imebaini kuwa ujenzi wa miradi ya maendeleo hususan ujenzi wa barabara unaathiri miundombinu ya maji kwa kiasi kikubwa.

iv. Baadhi ya maeneo ya ardhi kuna changamoto za kijiografia hali iliyopelekea ugumu katika uchimbaji wa visima.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu zaidi katika utanuzi wa bandari ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na vifaa.
ii. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba taasisi zote zenye miundombinu katika eneo ambalo mradi wa maendeleo unataka kutekelezwa zinashirikishwa kwa wakati ili kujadiliana kila hatua ya utekelezaji pamoja na kutatua changamoto iwapo zitajitokeza.
iii. Kwa upande mwengine Kamati inaishauri ZAWA husika kufanya tafiti za kimazingira kabla ya kuanza miradi ili kukwepa changamoto ambazo zinapelekea uzoroteshaji wa miradi.
iv. Kamati pia inaendelea kutoa msisitizo kwa Serikali kuhusiana na upatikanaji wa fedha kwa kuhakikisha unakwenda sambamba na kazi zilizopangwa.

## PROGRAMU YA KUIMARISHA VIWANJA VYA NDEGE

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ikishirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar katika kuimarisha huduma za usafiri wa anga imepanga kutekeleza miradi miwili ambayo itahusisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Nungwi pamoja na ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, kwa upande wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Nungwi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 6.6 bilioni lakini hadi na hadi kufikia Septemba 2023, hakuna fedha iliyotumika. Na kwa upande wa kiwanja cha ndege cha Pemba ulipangiwa jumla ya TZS 160 bilioni ambapo jumla ya TZS 10 bilioni ni kutoka Serikalini kwa ajili ya malipo ya fidia na TZS 150 bilioni ni kutoka kwa Mfadhili, na hadi kufikia Septemba 2023, hakuna fedha iliyotumika.

Ujenzi huo unategemewa kuanza rasmi mara tu baada ya kukamilika kwa mazungumzo baina ya Serikali na wahusika wa ujenzi.

### Changamoto Zilizobainika

i. Mamlaka inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa fedha kwa ajili ya

utekelezaji wa miradi hii.

ii. Uchelewaji wa tathmini ya vipango na majengo umepelekea Mamlaka kushindwa kuwalipa fidia wananchi watakaopishaa ujenzi wa kiwanja cha ndege Pemba.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Mamlaka kufuatilia kwa karibu kwa mtathmini mkuu ili kujua hatua iliyofikia kuhusiana na malipo ya wananchi.

ii. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha taratibu za malipo kwa ajili ya kuanza kwa ujenzi wa kiwanja cha ndege Pemba ili kutatua changamoto ya usafiri kwa upande wa Pemba.

## MRADI WA UJENZI WA NYUMBA ZA WAFANYAKAZI KATIKA HOSPITALI ZA WILAYA NA MKOA

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali za Wilaya na Mkoa ni miongoni mwa Miradi ya kimkakati iliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026. Mradi huu una lengo la kuimarisha utowaji wa huduma katika hospitali za wilaya na Mkoa ambapo unahusisha ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Pangatupu, Mwera Pongwe, Kitogani na Lumumba kwa upande wa Unguja na Vitongoji na Kinyasini kwa upande wa Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Afya imepanga kutumia jumla ya TZS 20,000,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuchelewa kupatikana kwa fedha kwa wakati uliopoangwa, kumepelekea kutokuanza kwa hatua za awali za utekelezaji wa miradi hii.

ii. Kamati imebaini kuwa kukosekana kwa upembuzi yakinifu kumepelekea

baadhi ya Hospitali zilizojengwa kuanzakufanya nyufa.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Wizara ya Afya kabla ya kuanza kwa miradi ni vyema kuzingatia kwa kina tathmini ya mazingira ili kuepuka gharama ambazo zinatokana na athari zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi.

ii. Kamati inaishauri Wizara kuongeza muda wa mradi kutokana na uchelewaji wa hatua za awali.

iii. Kwa kuzingatia umuhimu wa huduma za afya nchini, Kamati inaishauri Serikali kuipa kipaumbele miradi ya afya kwa kuingiza fedha za miradi kwa wakati ili iweze kukamilika katika muda uliyopangwa.

### PROGRAMU YA UJENZI WA BARABARA KUU PAMOJA NA UJENZI WA BARABARA ZA NDANI

Katika Kuimarisha Huduma za Usafiri wa Barabarani kwa upande wa Pemba na Unguja, Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani pamoja na Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu zimeanzishwa. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu imepangiwa jumla ya TSZ 206.39 bilioni ambapo jumla ya TZS 14 bilioni ni kutoka kwa wafadhili ambao ni BADEA/SAUDI FUND na TZS 160 bilioni ni kutoka UKEF na TSZ 32 bilioni ni mchango kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya malipo ya fidia. Ujenzi huu unahusisha barabara ya Wete - Chake yenye urefu wa kilomita 22.1 ambapo hatua iliyofikia ni ujazaji wa kifusi kwa urefu wa kilomita 13.5 kwa matabaka mbali mbali. Hatua ya ujenzi huu imefikia asilimia 20 ya utekelezaji.

Kwa upande wa Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani imepangiwa jumla ya TZS 44.06 bilioni, hadi kufikia Septemba 2023, TZS 8.075 bilioni zimetumika.

Programu hii inajumuisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 275.9 Unguja na Pemba ili kuwaondoshea wananchi changamoto ya usafiri iliyopo hivi sasa katika maeneo mbali mbali ya mjini na vijijini. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya ASER na IRIS kutoka nchini uturuki. Kwa kipindi cha Julai-Septemba 2023/2024 hatua ya ujenzi iliyofikia ni uwekaji wa kifusi tabaka la pili kwa baadhi ya maeneo.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Baadhi ya wananchi ambao wamepisha ujenzi hawakuridhishwa na kiwango cha fedha ambacho wamelipwa fidia ili kupisha ujenzi wa barabara

ii. Kuna baadhi ya miradi inayoendelea kusababisha kuharibika kwa miundombinu mengine ambayo inapatikana sehemu ambayo miradi ya ujenzi inatekelezwa.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kupitia na kufanya marekebisho ya kanuni za ulipaji fidia ili ziendane na hali halisi ya sasa ili kupunguza malalamiko ya mara kwa mara.

ii. Kamati inaishauri Serikali katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara kwenda sambamba Mpango Mkuu wa usafirishaji ili kuepusha changamoto ambazo zinaweza kutokea.

**PROGRAMU YA UJENZI WA OFISI ZA SERIKALI**

Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali inatekelezwa na Ofisi ya Rais -Fedha na Mipango. Lengo la program hii ni kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi ili kuweza kutoa huduma bora kwa wananchi katika maeneo yaliyopendekezwa pamoja na kufanya ukarabati katika baadhi ya majengo

ambayo yamechakaa.

Programu hii imepangiwa jumla ya TZS 74.122 bilioni kutoka Serikalini. Kati ya fedha hizo, TZS 19.044 bilioni ni kwa ajili ya utanuzi na ujenzi wa baadhi ya ofisi, na TZS 55.078 bilioni ni kwa ajili ya ujenzi wa mji mpya wa Serikali katika eneo la Kisakasaka.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kukosekana kwa hati miliki katika baadhi ya maeneo ni changamoto inayopelekea kuchelewa kuanza kwa baadhi ya miradi.

ii. Kukosekana kwa maeneo ya kufanyia kazi kwa muda kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Mufti Mkuu, kumepelekea wafanyakazi hao kukaa katika jengo linalofanyiwa ukarabati huku wakiendelea na majukumu yao hali iliyopelekea kukaa kwa tahadhari na kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa uafanisi.

iii. Baadhi ya maofisi kushindwa kupata fedha kwa mujibu wa makadirio yao waliyoyaweka na kupelekea kuongezeka kwa muda wa ukamilishaji wa miradi inayotekelezwa.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali, taasisi zote zinapokuwa zinatekeleza miradi mbali mbali kuhakikisha wanapokea kutoka kwa Mshauri Elekezi ili kuepuka gharama za ziada na kupelekea kuongezeka kwa muda wa ukamilishaji wa mradi.

ii. Upatikaji hati miliki imekuwa ni tatizo kwa baadhi ya taasisi, hivyo Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha upatikanaji wa hatimiliki unapangiwa utaratibu maalum ili kurahisisha utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

iii. Kamati inaishauri Serikali, vitengo vya ufuatie kwa karibu miradi yote ili iweze kukamilika kwa wakati.

iv. Kamati pia inaishauri Serikali kupanga miradi michache ambayo itaweza kutekelezeka kwa wakati kwa mujibu wa fedha zilizopo.

## MPANGO WA UNUNUZI WA VYOMBO VYA USAFIRI (GARI)

Kwa lengo la kutatua changamoto ya usafiri kwa watendaji na watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakiwemo Wakurugenzi na Makatibu Tawala kwa Wizara na Taasisi za Serikali, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ilipewa jukumu la ununuzi wa gari zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya Dola za Kimarekani 8.781 milioni sawa na TZS 22.041 bilioni zilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa gari hizo. Katika kufanikisha hili, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango iliingia mkataba na kampuni nne tofauti kwa ajili ya usambazaji wa gari hizo kwa matumizi ya Viongozi pamoja na Taasisi za Serikali. Baadhi ya gari hizo zimeshafika na nyengine zinatarajiwa kufika hivi karibu kupitia kampuni tofauti ambazo zilizoingiwa mkataba kwa ajili ya ununuzi huo. Kampuni hizo ni SAS AFRICAN GENERAL TRADING, BUCKET TANZANIA LIMITED, TATA AFRICAN HOLDINGS (TANZANIA) LIMITED, ZENJ MOTORS. Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango iliamua kuvunja mkataba na kampuni ya ZENJ MOTORS kutokana na kushindwa kuleta gari kwa mujibu wa makubalino, ikaamua kuingia mkataba na kampuni nyengine ya FKGS AUTOMOBILES LTD kwa ajili ya ununuzi wa magari.

### Changamoto Zilizobainika

i. Uhaba wa dola kwa baadhi ya kampuni kumepelekea kuchelewa kufika kwa gari kwa kipindi kilichotarajiwa.

ii. Taratibu za usafirishaji pia zimepelekea kutokufika kwa wakati kwa gari zilizokusudiwa.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kuingia mikataba na Kampuni ambazo zimekidhi vigezo na masharti ili kuepuka uchelewaji wa vyombo hivyo vya usafiri.

ii. Katika jitihada za kurahisisha upatikanaji wa bidhaa na vifaa mbali mbali kutoka nchi za nje, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na juhudi za kuimarisha utendaji wa bandari pamoja na kuwa na wafanyakazi wa kutosha.

## MRADI WA MJI SALAMA

Mradi wa mji salama Zanzibar ni mradi endelevu ambao umepangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Fedha ambazo zimepangwa kutekelezwa mradi huu ni TZS 1.5 bilioni kazi zilizofanyika katika mradi huu ni matengenezo ya miundombinu ambayo yamegharimu TZS 909.766 milioni pamoja na ununuzi wa kifaa aina ya 'SNOCKER' kwa gharama za TZS 142 milioni. Matengenezo ya miundombinu hiyo ni pamoja na matengenezo ya kamera 835 zilizopo katika kituo kikuu cha Maisara.

### Changamoto Zilizobainika

i. Kuondoshwa kwa muda mrefu kwa miundombinu ya kamera za ulinzi ili kupisha ujenzi wa barabara.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara, kurudishwa kwa miundombinu ya kamera iliyoondolewa kwa baadhi ya maeneo ili shughuli za ulinzi na usalama ziweze kuendelezwa.
ii. Kamati inaishauri Serikali, kuweka wafanyakazi wa kutosha ili vyumba vya kuangalia matukio (control rooms) ili shughuli za ulinzi na usalama ziweze

kutekelezwa kwa ufanisi.

## MRADI WA UJENZI WA OFISI ZA MASHEHA ZANZIBAR

Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Masheha umepangwa kuanza kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Mradi umepangiwa jumla ya TZS 3 bilioni. Kwa kipindi cha Julai- Disemba 2023, kazi zilifanyika katika mradi huu ni kumtafuta mkandarasi ambae ni kikosi cha Valantia Zanzibar na maombi ya malipo ya mkandarasi tayari yameshapelekwa Tume ya Mipango, kinachosubiriwa ni malipo na hatimae na kukabidhiwa eneo la mradi. Jumla ya ofisi ambazo zitajengwa ni 64, 40 kwa upande wa Unguja na 24 kwa upande wa Pemba.

### Changamoto Zilizobainika

i. Mradi kuchelewa kuanza kutokana na utaratibu wa upatikanaji wa fedha za maendeleo.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ itakapoanza ujenzi wa ofisi za masheha kuzingatia mazingira husika ya makaazi ya masheha hao ili kuwezesha ofisi hizo kufikiwa na wananchi kwa ajili ya kupata huduma kufika ofisini.

ii. Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa kuanda mpango wa kuwapatia vitendea kazi kulingana na mahitaji yao ili kuwafanya masheha hao kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## MRADI WA UJENZI WA NYUMBA NA MAHANGA YA CHUO CHA MAFUNZO

Chuo cha Mafunzo kwa mwaka 2017/2018 kiliaanza kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga kwa lengo la kupunguza changamoto ya makaazi kwa wapiganaji katika kambi za Unguja na Pemba. Chuo cha Mafunzo ilianza

utekelezaji wa mradi huo kwa kuanza ujenzi kambi za Tungamaa, Kengeja, Kangagani na kwa sasa kuendelea na kambi ya Wete pamoja na kambi zilizobakia za Unguja.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Chuo cha Mafunzo ilipanga kutumia jumla ya TZS 2.23 bilioni katika shughuli za kimaendeleo na hadi kufikia June 2022 fedha iliyoingia ni TZS 2.23 bilioni sawa na asilimia 100% ya fedha ya Mradi ambapo TZS 1.73 bilioni zilipangiwa kutumika kwa ujenzi wa jengo la ofisi ya Makao Makuu Unguja na TZS 500 milioni kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wete - Pemba.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kutopata fedha kwa wakati za kutekeleza miradi ya kimaendeleo iliyopangwa.
ii. Kuongezeka kwa bei za vifaa vya kujengea.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kuhakikisha miradi ya maendeleo iliyoanza kutekelezwa inapewa kipaumbele kwa kuingiziwa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi hiyo kwa muda uliopangwa ili kuepukana na tatizo la kuongozeka kwa bei za vifaa vya ujenzi.

## PROGRAMU YA KUIMARISHA VIWANJA VYA MICHEZO

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilitengewa jumla ya **TZS 34.2 bilioni** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo kama ifuatayo:

**Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya**

Mradi huu ulipangiwa TZS 12 bilioni na hadi kufikia Disemba 2023 viwanja 35 vya michezo Unguja n Pemba vimepimwa ila hakuna fedha iliyotumika kwenye

utekelezaji wa mradi.

**Mradi wa Uimarishaji (Ukarabati) wa Viwanja vya Michezo**

Jumla ya TZS 21 bilioni zilitengwa kupitia Wizara na Serikali kwa upande wake iliongeza TZS 50 bilioni kwa kuona umuhimu wa michezo na ubora wa miundombinu yake. Uwanja wa Amani Unguja ulitengewa jumla ya TZS 55 bilioni na hadi kufikia Disemba 2023 jumla ya TZS 45 zimeshatumika. Kwa upande wa uwaja wa Gombani Pemba ulitengewa jumla ya TZS 5.6 bilioni na hadi kufikia Disemba 2023 jumla ya TZS 3.9 bilioni zimeshatumika

**Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo midogo midogo (4 in1)**

Mradi huu ulipangiwa jumla ya TZS 1.2 bilioni na hadi kufikia Disemba 2023 jumla ya TZS 150 milioni zimetumika.

**Changamoto Zilizobainika**

Katika kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo kamati imeabini changamoto zifuatazo:

i. Kuchelewa kuingiziwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.
ii. Mradi kutokamilika kwa wakati uliopangwa.
iii. Mipango ya uendeshaji wa uwanja baada ya kukabidhiwa rasmi bado haijapangwa rasmi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kuipatia fedha Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo ili imalizie miradi iliyokuwa bado haijamaliza ili kufikia malengo ya kuimarisha viwanja vya michezo.
ii. Kamati inaishauri Wizara kuandaa kuandaa utaratibu wa uendeshaji wa viwanja.
iii. Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Michezo kutoa elimu kwa wananchi na watumiaji mbali mbali wa viwanja juu ya matumizi sahihi na

utunzaji wa viwanja hivyo.

## MRADI WA BANDARI JUMUISHI MANGAPWANI

Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 inaendelea na harakati za ujenzi wa Mradi wa Bandari Jumuishi Mangapwani wenye eneo la hekta 930. Mradi huu unajumuisha Bandari ya Mizigo mchanganyiko, Chelezo, Bandari ya mafuta na gesi, eneo la matenki ya kuhifadhia mafuta na gesi, eneo la makontena na maghala, eneo la viwanda na biashara, pamoja na eneo la makazi. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya TZS 20 bilioni zimetengwa kwa ajili ya miundombinu ya barabara itakayopita kwenye eneo la mradi wa bandari jumuishi na hadi kufikia disemba 2023 jumla ya TZS 12.9 bilioni zimetumika kwa kumlipa mkandarasi na fidia kwa wananchi.

### Changamoto Zilizobainika

i. Wakandarasi wa ujenzi wa barabara kushindwa kuendelea na kazi zao vizuri kwa sababu bado wananchi hawajakubali kuondoka.
ii. Kutokuwepo kwa fidia ya ardhi kitu ambacho kimepelekea ugumu kwa wananchi kukubali kwani wanalipwa fidia ya vipando na majengo pekee.
iii. Kuchelewa kwa malipo ya fidia ya vipando na majengo.
iv. Baadhi ya maeneo ya mradi kuwepo kwa makaburi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inashauri Wizara na Taasisi nyengine inazoshirikiana nazo kufanya uchambuzi na kupitia mapendekezo ya wawekezaji na wajenzi kwa umakini ili kutatua changamoto zote zinazoibuka wakati wa kutekeleza mradi huu muhimu kwa nchi yetu.

ii. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inajenga nyumba zenye viwango na zitakazokidhi mahitaji ya wananchi ambao watalipwa nyumba hizo kama fidia ya majengo.

iii. Kamati inaishauri Serikali na Wizara kuhakikisha inaongeza jitihada ya kukaa pamoja na wananchi ili kutatua changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi huu.

# SEHEMU YA SABA

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

### Tathmini ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bajeti kwa Mabaraza ya Miji na Manispaa kwa Upande wa Pemba

Katika kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa maoni na ushauri wa uliotoa kwenye ripoti ya Kamati ya Febuari 2023 kwa Mabaraza ya Miji na Halmashauri kwa upande wa Pemba. Hatua hii ni kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati ya Bajeti umefanyika katika miradi ya vituo vya wajasiriamali, masoko, vituo vya daladala na kumbi za mikutano kwa upande wa Pemba kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, Baraza la Mji Wete, Baraza la Mji Mkoani na Manispaa ya Chake Chake.

Kamati ya Bajeti imebaini changamoto mbalimbali ilipotembelea maeneo husika ya miradi.

**Changamoto Zilizobainika**

i. Kituo cha wajasiriamali Tumbe kutotumiwa na wajasiriamali kutokana na tatizo la kutokuwepo kwa wateja wa uhakika na kupelekea maduka mengi kufungwa.

ii. Wajasiriamali wanalalamika kwa kutopatiwa mkopo kwa ajili ya mtaji kutoka benki ya CRDB kama walivyoahidiwa na kujaza fomu.

iii. Katika kituo cha daladala Kinowe – Konde wafanyabiashara waliokuwepo ni wachache na wengi wao wamebakia maeneo yao ya awali Stendi ya Konde na kupelekea kituo hicho kutotumika ipasavyo kwa wafanyabiashara.

iv. Ukosefu wa maji, vyoo na mahema kwa ajili ya wajasiriamali kujihifadhi ili kujikinga na jua na mvua.

v. Changamoto ya vyanzo vya mapato kwa halmashauri na manispaa na mabaraza ya miji kutokuwa vya uhakika na kukidhi haja ya kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na mapato wanayokusanya hivyo kupelekea kutekeleza miradi kwa mikopo ambayo inawapa ugumu katika ulipaji.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i. Kamati inazishauri Halmashauri, Mabaraza ya Miji na Manispaa kuhakikisha miradi mikubwa ya kimkakati inapoandaliwa kujumuisha kila kitu kwa mahitaji ya watumiaji.

ii. Kamati inazisisitiza Halmashauri, Mabaraza ya Miji na Manispaa kuharakisha upatikanaji wa mikopo kwa wajasiriamali kama zilivyoahidi, vile vile kuhakikisha inachukua jitihada za kutengeneza mazingira ya kuwahamishia wafanyabiashara na wajasiriamali kwenye maeneo

yaliyotengwa rasmi.

iii. Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya vyanzo vya mapato vya Halmashauri, Mabaraza ya Miji na Manispaa kwa kuzisaidia njia za kupata fedha ili ziweze kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati.

iv. Kamati inazishauri Halmashauri, Mabaraza ya Miji na Manispaa kuhakikisha zinaondokana na changamoto ya muingiliano wa majukumu ya kiutendaji na Ofisi za Wakuu wa Mikoa ili kuleta ufanisi kiutendaji.

v. Kamati inazishauri Halmashauri, Mabaraza ya Miji na Manispaa kuhakikisha masoko, vituo vya wajasiriamali na vituo vya daladala vinatunzwa ili kuwanufaisha wananchi kwa muda mrefu.

# SEHEMU YA NANE

## HITIMISHO

Naomba nihitimishe ripoti hii kwa kumshukuru Spika Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa kuwa makini katika kuliongoza Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza majukumu yake vyema na kwa uweledi mkubwa akisaidiwa na wasaidizi wake Mheshimiwa Naibu Spika Mgeni Hassan Juma pamoja na wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi. Aidha, shukurani za dhati ziende kwa Mheshimiwa Dkt Saada Mkuya Salum, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango pamoja na watendaji wake mbali mbali waliopo katika taasisi anazozisimamia kwa mashirikiano yao makubwa waliyoipatia Kamati kwa muda wote wa kutekeleza majukumu yake.

Kwa upande mwengine, Kamati haina budi kuwashukuru Mawaziri, Manaibu mawaziri, Makatibu wakuu, Wakurugenzi, Maafisa Wadhamini pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi za Serikali ambazo ilipata fursa ya kukutana nao katika utekelezaji wa majukumu yake. Ni matarajio yetu kuwa, maeneo yote ambayo Kamati iliyapitia yaliweza kupatiwa maoni na ushauri ambao uliwasaidia katika kufanikisha shughuli zao.

Ifahamike kwamba kukamilika kwa ripoti hii pia kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na mashirikiano waliyoyatoa wajumbe wa Kamati ya Bajeti ambao kwa umoja wao walitekeleza majukumu ya Kamati kwa umakini mkubwa na kupelekea kukamilika kwa ratiba zote za Kamati zilizopangwa kwa wakati.

Mwisho, Kamati inaishukuru kwa dhati kabisa Afisi ya Baraza la Wawakilishi na watendaji wake wote ambao waliweza kuisaidia Kamati kufanikisha kazi zake katika vipindi mbali mbali vya utekelezaji wa majukumu yao. Ni matarajio ya

Kamati kuwa, maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa katika ripoti hii utafanyiwa kazi ipasavyo na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Naomba kutoa hoja.